# Nipashe

Jumamosi Machi 27, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580532

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper LIKE & FOLLOW US

**Askofu** Nyaisonga awapa ujumbe mzito viongozi msibani

UKURASA 3



**JK** afichua kuingia na majina matano 'vita' ya urais CCM

UKURASA 4



Costa atua rasmi Benfica

UKURASA 21

# MWISHO WA ENZI

• **Hatimaye** Magufuli azikwa rasmi Chato... *Endelea ukurasa 2*



Rais Samia Suluhu Hassan, akiweka shada la maua kwenye kaburi la Hayati Dk. John Magufuli, baada ya maziko yaliyofanyika nyumbani kwake, Kijiji cha Mlimani, Chato mkoani Geita jana. **Picha zingine:** Mjane wa Dk. Magufuli, Janeth Magufuli na watoto wakiweka mashada ya maua. **Picha zaidi Uk. 7 na 18. PICHA: MAELEZO**

## Mabeyo: Nilipewa ujumbe na JPM

UKURASA 4

**MICHEZO** GAUCHO RASMI ASAJILIWA MOROCCO UK.23 **MAONI, KATUNI** UK.6



Rais mstaafu, Ali Hassan Mwinyi na mkewe Sitti Mwinyi, wakiweka shada la maua kwenye kaburi la Hayati, Dk. John Magufuli, baada ya maziko yaliyofanyika nyumbani kwake, Kijiji cha Mlimani, Chato, mkoani Geita jana. **PICHA: MAELEZO**

# Mwisho wa enzi, JPM azikwa

**Na Richard Makore, CHATO**

MWISHO wa enzi. Hivyo ndivyo inavyoweza kuelezwa kutokana na kutamatika kwa safari ya aliyekuwa Rais wa Awamu ya Tano wa Tanzania, Dk. John Magufuli.

Magufuli aliyefariki dunia Machi 17, mwaka huu, katika Hospitali ya Mzena, Dar es Salaam, alizikwa jana nyumbani kwao, kijijini Mlimani, Chato mkoani Kagera. Maziko ya kiongozi huyo yalihudhuriwa na mamia ya watu wakiongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan.

Viongozi wengine waliohudhuria maziko hayo yaliyotanguliwa na ibada iliyofanyika katika uwanja wa Mpira wa Magufuli ni Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi; Waziri Mkuu Kassim Majaliwa; Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman; Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla; Jaji Mkuu wa Tanzania, Profesa Ibrahim Juma na Spika wa Bunge la Tanzania, Job Ndugai.

Wengine ni marais wastaafu wa Tanzania, Mzee Ali Hassan Mwinyi na Dk. Jakaya Kikwete; Rais Mstaafu wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein; Katibu Mkuu Kiongozi, Dk. Bashiru Ally, na Katibu Mkuu Kiongozi Zanzibar, Mhandisi Zena Ahmed Said na wakuu wa vyombo vya ulinzi na usalama wakiongozwa na Mkuu wa Majeshi, Jenerali Vanance Mabeyo.

Pia mjane wa Magufuli, Mama Janet, watoto, wajukuu wanafamilia na viongozi wakiwamo mawaziri, naibu mawaziri, makatibu wakuu, naibu makatibu wakuu na viongozi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) wakiongozwa na Makamu Mwenyekiti Bara, Philip Mangula walihudhuria.

Maziko hayo yaliyofanyika kwenye makaburi ya familia nyumbani kwao, Magufuli alizikwa kwa heshima zote za kitaifa na za kijeshi pamoja na taratibu za kidini chini ya Kanisa Katoliki, ambalo alikuwa muumini wake.

**MISA TAKATIFU**

Kabla ya maziko, kulifanyika misa takatifu katika Uwanja wa Mpira wa Magufuli, iliyoongozwa na Rais wa baraza la maaskofu wa Kanisa Katoliki (TEC), Mhashamu Askofu Mkuu Gervas Nyaisonga, akisaidiwa na maaskofu wakuu na maaskofu wa kanisa hilo kutoka majimbo mbalimbali.

Mwili wa Hayati Magufuli uliwasili uwanjani hapo saa 3.40 asubuhi na kupokewa na viongozi mbalimbali na wananchi wa maeneo ya jirani.

Hata hivyo, baadhi ya wananchi na waombolezaji walianza kuingia uwanjani hapo kuanzia saa 11 asubuhi na kwenda kukaa maeneo waliyoelekezwa na vyombo vya ulinzi na usalama.

Tofauti na siku zingine tangu msiba huo utangazwe, jana hapakuwa na vilio kwa waombolezaji katika misa hiyo ambayo ilihudhuriwa na zaidi ya maaskofu 10, muda wote wa misa, wananchi walikuwa wamekaa kwa utulivu.

Licha ya jua kali kuwaka katika uwanja huo, wananchi walivumilia mpaka shughuli yote kumalizika zikiwamo hotuba za viongozi wa chama na serikali.

Kwa upande wa nyumbani kwa hayati Magufuli, wananchi mbalimbali ambao ni majirani zake walionekana pembezoni huku wakiwa na huzuni na simanzi.

**MAZIKO RASMI**

Baada ya kumalizika kwa misa iliyoambatana na salamu na hotuba mbalimbali kutoka kwa viongozi, msafara kutoka uwanjani kwenda nyumbani ambako ndiko alikozikwa ulianza.

Waombolezaji wakiongozwa na Rais Samia waliingia katika eneo la kaburi na kukaa kisha gwaride maalum la kijeshi lilifuata kuingiza mwili ndani.

Jeneza lililobeba mwili wa Hayati Magufuli, liliingia nyumbani kwake kutokea uwanjani saa 10.25 jioni, likiwa limebebwa na maofisa waandamizi wa JWTZ wenye vyeo vya kanali huku brass band ya JWTZ ikiongoza msafara uliokuwa kwa mwendo wa pole.

Hatimaye saa 10:48 mwili wa Hayati Magufuli uliingizwa kaburini na maofisa wakuu wa JWTZ wenye vyeo vya brigedia jenerali. Baada ya hapo, ilianza sala ya maziko iliyoongozwa na Askofu wa Kanisa Katoliki wa Jimbo la Rulenge Ngara, Severine Niwemugizi. Kabla ya kuingizwa mwili kaburini, Askofu Niwemugizi aliliombea kaburi.

Aidha, maziko hayo yalitawaliwa na ndege za vita za kijeshi ambazo zilikuwa zikipita juu ikiwa ni ishara kwamba anayehifadhiwa katika nyumba yake ya milele alikuwa Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama.

Katika kipindi chote watu wachache waliohudhuria maziko hayo, walionekana watulivu na hapakuwa na vilio kama ilivyokuwa siku zingine. Hata hivyo, Rais Samia alishindwa kujizuia kwa kuwa wakati mwili ukishushwa kaburini, alitokwa na machozi.

Katika eneo hilo la maziko vyombo vya ulinzi na usalama vilionekana kufanya kazi yao kwa umakini ili kuhakikisha kila mtu anayeingia hapo anakaa katika mpangilio. Eneo lote linalozunguka nyumbani kwa hayati Magufuli lilikuwa tulivu na zilisikika sauti za ndege zilizotokea katika miti iliyozunguka kwake.

**MIZINGA YAPIGWA**

Baada ya kukamilika kwa maziko, hatua iliyofuata ni kupigwa kwa mizinga 21 na kikosi maalum cha JWTZ kuashiria kuwa aliyezikwa alikuwa Amiri Jeshi Mkuu.

## Samia atoa msimamo Chato kuwa mkoa

**Na Romana Mallya**

RAIS Samia Suluhu Hassan, ameagiza mchakato wa Chato kuwa mkoa uharakishwe ili ndoto ya Rais John Magufuli itimie.

Aliyasema hayo jana katika misa ya maziko ya mwili wa Rais Magufuli na kubainisha kuwa ana taarifa za mchakato huo kuanza.

"Ninaagiza mchakato umalizike katika ngazi ya huko na muulete serikalini ili kama vigezo vimekidhi kuwa mkoa peke yake, hatuna budi kufanya hivyo. Kama vigezo havijakidhi, tutaelekeza wafanye nini ili vikidhi ili lifikie lile lengo lenu.

"Lakini, kwa ajili ya kumuenzi kiongozi wetu, niwaombe mkamilishe, tuone namna tutakavyoweza kufanya," Rais Samia alisema.

Kuhusu tatizo la upungufu wa dawa wilayani Chato lililoibuliwa na mmoja wa wazee wa wilaya hiyo wakati wa misa hiyo, kiongozi huyo wa nchi aliahidi kulibeba na kulifanyia kazi ili kuhakikisha linatatuliwa.

Alisema anatambua kwamba miaka mitano iliyopita, serikali iliondoa kwa kiwango kikubwa tatizo hilo kutoka asilimia 35 ya upatikanaji wa dawa hadi asilimia 94 kitaifa.

"Kama Chato haipati dawa, kuna tatizo katikati ambalo lazima lifanyiwe kazi. Niwaahidi tutalifanyia kazi na dawa zitapatikana," alisema.

Rais Samia aliwahakikishia wana Chato na Watanzania kuwa kinachofuata ni kutekeleza ahadi zote zilizoko ndani ya ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) na zile alizozitoa Hayati Rais Magufuli kwa watu wake.

"Hili siyo kwa watu wa Chato pekee, hata kwa mikoa yote ya Tanzania, imesemwa vizuri hapa tumempoteza jemedari wetu, shujaa wetu, lakini aliyotufundisha na wasaidizi wake tupo, tutachapa kazi," aliahidi.

Rais Samia aliishukuru familia ya Rais Magufuli pamoja na ofisi binafsi kwa ushirikiano walioutoa kipindi chote cha kuugua hadi umauti ulipomfika kiongozi huyo na kuwataka wanafamilia kumwelekea Mungu ili awashike mkono.

"Leo (jana) tunampumzisha baba, shujaa, jemedari wetu, tumuombee pumziko la amani na amani ya milele. Watanzania, Rais Magufuli ameitwa na Mungu na ameitika, leo (jana) tunakwenda kumsitiri.

"Tunachokwenda kukisitiri ni kiwiliwili chake, lakini maono na falsafa yake ya hapa kazi tu itaendelea kuwapo na kuifanyia kazi.

"Niwaombe sana watu wote tunaotoa huduma kwa wananchi serikalini lakini pia taasisi binafsi na hata viongozi wa dini twende kuonyesha mshikamano, ushirikiano, upendo kwa taifa letu.

"Kama kuna muda wa kuonyesha upendo kwa taifa, ni muda huu ambao tumeondokewa na jemeradi wetu. Basi tusiyumbe wala kuliyumbisha taifa, twendeni tukaonyeshe upendo, mshimamano, tukaliendeleze taifa la Tanzania," alisema.

Rais Samia alisema kuwa jana ilikuwa mara yake ya tatu kwenda Chato na mara ya mwisho alikwenda baada ya Rais Magufuli kufiwa na dada yake ambapo wakati wakiwa huko, alimwonyesha eneo ambalo wanafamilia huzikwa.

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, aliwashukuru Watanzania kwa kujitokeza kwa wingi maeneo yote ambako mwili wa Rais Magufuli ulipitishwa kuanzia Machi 20 mkoani Dar es Salaam hadi Chato.

"Tunatambua kwa miaka miwili mama mzazi wa Rais Magufuli bado yupo kitandani, lakini Rais nimetekekeza agizo lako la kutaka madaktari wanaomhudumia waendelee kumhudumia bibi yetu mpaka hapo atakaporejea katika hali yake ya kawaida, wataendelea kumhudumia," alisema.








Viongozi wa dini wakiendesha ibada ya maziko ya Hayati Dk. John Magufuli, katika Uwanja wa Magufuli, wilayani Chato, mkoani Geita jana. **PICHA: MAELEZO**

# Askofu Nyaisonga awapa ujumbe mzito viongozi

**Na Romana Mallya**

RAIS wa Baraza la Maaskofu Tanzania (TEC), Askofu Mkuu Gervas Nyaisonga, amesema Rais John Magufuli pamoja na maradhi ya moyo aliyokuwa nayo, hakuchoka kuwapigania Watanzania na amekufa akiwahangaikia kutoka katika aibu ya umaskini.

Vilevile, kiongozi huyo wa kiroho aliwataka viongozi kuwa na msimamo mkali katika baadhi ya masuala yakiwamo yanayohusu haki za binadamu ili kulinda utu na heshima ya taifa.

Aliyasema hayo jana katika misa ya maziko ya mwili wa Rais Magufuli iliyofanyika kwenye Uwanja wa Magufuli wilayani Chato mkoani Geita na kuhudhuriwa na Rais Samia Suluhu Hassan, Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, na viongozi wa serikali, wakuu wa majeshi ya ulinzi na usalama, viongozi vyama vya siasa, dini na wananchi.

Baada ya misa hiyo na ya awali iliyofanyika kwenye Kanisa Katoliki Chato, Rais Magufuli alipumzishwa kwenye nyumba yake ya milele katika makaburi ya familia nyumbani kwao, Chato.

"Tunachekwa kila mahali, Tanzania ni maskini, Uganda maskini, Afrika maskini. Hayati Rais Magufuli alipenda, tena kwa nguvu zote tujikomboe na aibu ya kunyonywa.

"Hakuwa kama wale wachungaji wa nyakati za Yeremia na Ezekiel. Wao waliwaacha kondoo wao katika mazingira magumu, tena ya mbwa mwitu, wachungaji wakakimbia na kondoo wakakimbia, wachungaji wakawatekeleza kondoo," alisema.

Alimshukuru Mungu Tanzania tangu ipate uhuru haijawahi kuingia katika mikono ya wachungaji waovu waliowatelekeza Watanzania.

"Watanzania wengi wamebaki katika nchi yao. Ni kitu cha kujipongeza na kumshukuru Mungu na kumpongeza Rais Magufuli na watangulizi wake.

"Wanaomjua zaidi wanasema alikuwa anakesha, mimi simjui ninasikia tu. Ninaamini alifanya hivyo siyo tu kwa faida yake na familia yake, bali kwa faida ya taifa letu.

"Hata wakati wa hofu kubwa ya corona ilipotanda sehemu nyingi za ulimwengu, alikuwa tayari kutofautiana na wengi kwa maslahi ya nchi na watu wake. Rais Magufuli hakueleweka, pia alitukanwa lakini alibaki imara," alisema.

### JANGA LA CORONA

Askofu Nyaisonga alisema sehemu mbalimbali wameanza kuwapigia simu wamechoka kukaa ndani kuogopa corona.

"Nadharia ya corona ni nadharia ya ajabu na wengi wanatuomba waje Tanzania. Ni kitu cha kumshukuru Mungu," alisema.

Aliwataka viongozi wajifunze kutoka kwa Rais Magufuli kwa kuwaeleza kuwa faida binafsi haijengi taifa, bali inaliumiza.

"Inaumiza wanyoge, tujitoe kwa moyo wetu wote na kwa nguvu zetu zote kama mtu huyu alivyojitoa. Rais Magufuli ameacha jambo lingine muhimu katika maisha la kumtegemea Mungu.

"Hakuogopa kutoa sifa na utukufu kwa Mungu, hakuogopa kutaja hata kusema kwamba tumtegemee Mungu na hata yeye tumwombee. Katika ulimwengu hasa wa leo, sehemu za Magharibi huko kumtegemea Mungu na kutajataja Mungu ni ushamba.

"Ni aibu wanasikia mtu anatajataja Mungu, wanaona huyu ni mjinga na Wakatoliki huwa tunafanya ishara ya msalaba kusali, wengi wanaona aibu hawafanyi, ukifanya hivyo mbele ya watu wewe umepitwa na wakati, wewe ni mshamba.

"Mataifa kadhaa yameshindwa hata kuweka bayana katika katiba zao zinazowaunganisha, lakini kwa sababu ya neno Mungu.

"Nchi fulani inasema tuweke neno 'Mungu', wengine wanakataa hakuna Mungu, ni upagani wa hali ya juu. Wanasema Mungu anatufaa nini katika maisha yetu? Ni wazi unaweza kuona mtu anatengeneza bomu la nyuklia, hivi unafikiri alisali na kutengeneza?" alihoji.

"Sasa inatokea katika nchi ya Tanzania mtu kama Magufuli yeye kila mara anataja neno Mungu na anahimiza hata watu wake wamwombee kwa Mungu, watu wale wanaona amechanganyikiwa badala ya kutegemea sayansi na utafiti, mtu huyu anamtegemea Mungu, wanashangaa, tumwombe Mungu tusiingie katika mazingira ya namna hiyo, tubaki waaminifu kwa Mungu," alisema.

### UJUMBE MZITO

Aliwataka Watanzania wafanye kazi kwa bidii na kumwomba Mungu kama ambavyo Rais Magufuli alivyokuwa akihimiza hilo kila mara.

"Hakuna maendeleo waliyopatikana bila mkono wa Mungu, mambo mengi tunayoyaona Ulaya na sehemu mbalimbali yametokana na kufanya kazi na kumtegemea Mungu," alisema.

"Tunaona utoaji wa mimba, ushoga na majuzi Amerika walipitisha sheria ya usawa, ni upuuzi! Tunaomba viongozi wetu tusije tukafika hapo, mnapokuwa bungeni, bungeni ni patakatifu, siyo kuanza kuzungumza mambo ya kipuuzi, watu wabadilishe jinsia, watoe mimba.

"Waliotoa mimba wanatamani kuzaa, hawawezi, alikunywa mama na bibi dawa za kuzuia mimba, anayeathirika ni mjukuu.

"Kuna baadhi ya nchi wanajaribu kuwapa fedha unapozaa mmoja tunza, wa pili tutatunza, wanajitahidi wala hawawezi, walihasi watu wale, ninaomba tusifikie hapo," alionya.

Askofu Nyaisonga alisema anamshukuru Mungu kwamba Rais Samia anaelewa maana ya mambo hayo na kumtaka asaidie na kusimama imara ili Tanzania ikiwezekana na nchi jirani, wanapoongea, isifikie hatua ya watu kubadili jinsia kwa kuwa ni upuuzi na kujidanganya.

Alisema ishara na alama alizoacha Rais Magufuli ni ushahidi tosha wa wingi wa miaka yake 61 ya kuishi, miaka sita kama mtawala ambaye ataishi miaka mingi.

Makamu wa Rais TEC, Askofu Flavian Kasalla, alisema TEC inatambua imeondokewa na mtu mwadilifu, mzalendo na mchapakazi na aliyetetea maslahi ya Watanzania hasa wanyonge ndani na nje ya nchi.

Alisema watamuenzi kwa mikakati mbalimbali ya kujenga uchumi wa nchi na juhudi za kuhimiza nidhamu ya kiutendaji kwa yeyote aliyekabidhiwa kuwatumikia wengine.

"Hii imekuwa siri kubwa ya taifa katika mapambano ya kujiletea maendeleo endelevu, kaulimbiu ya 'Hapa Kazi Tu' itakuwa mwanga na dira ya kutekeleza maisha bora ya kila Mtanzania.

"Rais Samia, maaskofu tunakuhakikisha sala zetu na ushirikiano katika kutekeleza majukumu uliyokabidhiwa katika taifa hili," alisema.

### BAKWATA

Sheikh Mkuu wa Tanzania, Mufti Abubakary Zubeir, alisema Rais Magufuli aliwapenda viongozi wa dini na sifa kubwa aliyokuwa nayo na kuionyesha kwa miaka sita ni mapenzi makubwa kwa viongozi wa dini na alikuwa hapendi kuwakosa katika shughuli zake.

"Yapo makubwa kwa upande wa Waislam, Rais Magufuli ana mambo mengi lakini machache kati yake kwa Waislam ni kuwapatia msikiti mkubwa wenye uwezo wa kuingia waumini wengi," alisema.

"Haya ni mahaba makubwa, alichangia ujenzi Msikiti wa Chamwino Dodoma na akataka uitwe Abubakar Zuberi, Rais Samia na wasaidizi wako msimame katika mirathi hii mliyoachiwa na Rais Magufuli kusukuma na kuendesha jahazi kwa usalama na amani," alisema.

### CCT

Mwenyekiti wa Jumuiya ya Kikristo Tanzania (CCT), Askofu Alinikisa Cheyo, alisema kazi kubwa aliyoifanya Rais Magufuli ni kuwaunganisha Watanzania kuwa kitu kimoja bila ubaguzi wa dini, ukabila, ukanda na ushahidi huo umo mioyoni mwa Watanzania wote.

Alisema dunia inajua Tanzania ni sehemu ya kujifunza umoja, amani na uzalendo na kumwahidi Rais Samia kumuunga mkono kwa kila hali katika utumishi wake na hawatamwacha peke yake.



Rais mstaafu Dk. Jakaya Kikwete, akiwa katika ibada ya maziko ya Hayati Dk. John Magufuli, katika Uwanja wa Magufuli, wilayani Chato, mkoani Geita jana. **PICHA: MAELEZO**

# JK aanika alivyoingia na majina matano 'vita' ya urais CCM 2015

**Na Romana Mallya**

RAIS wa awamu ya nne, Jakaya Kikwete, amefunguka alivyokwenda na majina matano ya wagombea urais likiwamo la Dk. John Magufuli katika vikao vya juu vya Chama Cha Mapinduzi (CCM) na kuyatetea kwanini mmoja kati yao apitishwe kati ya 38 waliojitokeza.

Alianika suala hilo jana wakati wa misa ya maziko ya mwili wa Rais Magufuli iliyofanyika Uwanja wa Magufuli wilayani Chato mkoani Geita.

Rais Kikwete, akimwelezea Hayati Dk. Magufuli, alisema katika mchakato wa kuomba ridhaa ya kugombea urais mwaka 2015, walijitokeza watu 38 na kazi yake ilikuwa kuwapunguza na kufikia watano.

"Katika majina matano niliyoyafikisha kwenye vikao vya juu vya chama, sikusita kumpendekeza Magufuli, sikuwa na tabu kwa Magufuli, lilikuwa ndiyo jina la kwanza halafu nikaongeza na wengine.

"Na majina yale unakaa nayo wewe mwenyewe siri yako, wapo waliokuwa wanakuja kina Mzee Philip Mangula, vipi mambo yanakwendaje, fulani vipi, fulani usimweke, ninamwambia nimesikia.

"Majina yale niliyatoa kwa mara ya kwanza kwenye Kamati ya Usalama na Maadili ya CCM, mjadala mkali uliibuka 'kwa nini umemwacha fulani? ulioleta wote hawatoshi, wepesi'," alisema.

Rais Kikwete alisema walipokwenda kwenye Kamati Kuu ndiko kukawa na mjadala mkali na walilazimika kwenda hadi usiku wa manani na kazi ilikuwa ni yeye kujenga hoja 'kwa nini majina yale matano?'.

"Nikawaambia lazima ninayeondoka tukabidhi kizazi cha wadogo zetu, nilijitahidi wakati mwingine ukiwa Rais na Mwenyekiti una nguvu, tukakubaliana, tukaja NEC wee...!

"Tukaanza kwa kishindo lakini tukazungumza kwa hoja mpaka tukakubaliana majina ni yale hatuongezi wala kupunguza, tukapiga kura yakaja matatu," alisema.

Rais Kikwete alisema walipita katika vipindi vingine ambavyo ameviandika kwenye kitabu cha maisha yake anachokiandaa. Alisema wakati wa utawala wake, Dk. Magufuli alikuwa ni waziri pekee ambaye alikuwa na uwezo wa kumtania kama Rais na hata alipomkwaza, alipata ujumbe kupitia kwa kaka yake, Suleiman Kikwete (sasa marehemu).

Rais Kikwete alisema Dk. Magufuli akiwa mbunge na waziri, alimtunuku kiwanja Chato na alipokuwa Rais, alikiongeza na hati yake aliipata miezi miwili iliyopita na kumtaka ajenge.

Alisema Hayati Dk. Magufuli alikuwa waziri aliyemwamini na kumtumaini katika kipindi chake cha urais wa miaka 10 kwa sababu alikuwa 'jembe' ndiyo maana alimweka katika wizara tatu alizoziita ngumu.

"Nilimuweka Ardhi, nikawambia watu wanagawa viwanja mara nne nne, alipigana akafika mahali wale jamaa wagumu kweli, sijui kama Rais (Samia) utapata dawa ya watu wa ardhi, ukipata tutakushangilia," alisema.

"Nikampelekea Mifugo, nikasema tutoke kwenye kuchunga, twende kwenye kufuga, alifanya kazi nzuri. Alikuwa ananipiga hesabu ya samaki wangapi, wavuvi haramu waliona cha moto, samaki waliongezeka," alisema.

Rais Kikwete alisema alitaka akiondoka madarakani, watu wamkumbuke kwa barabara za lami za mikoa na ndipo alipomhamishia Wizara ya Ujenzi na alitekeleza kazi nzuri kwa miaka mitano ya mwisho wa utawala wa serikali ya awamu ya nne.

Rais wa awamu ya pili, Ali Hassan Mwinyi, alisema alihemewa na huzuni baada ya kutangazwa kwa kifo cha Rais Magufuli.

"Bado hajawa mzee, aliupata baada ya kuwa Rais, usiku ule sikupata usingizi kwa sababu mimi ni mpenzi mkubwa wa viongozi na Rais Magufuli ni mmojawapo wa viongozi na nilimpenda sana. Kwa dakika mbili nilikaa kimya, ninawaza.

"Rais alikuwa na fikra, mawazo na manufaa kwa taifa na Mungu anatuondoshea kijana mwenye manufaa kwa taifa lake, nilipata matatizo sana ya fikra, utadhania kijana hafi wanakufa wazee tu, habari hii ilinishtua sana," alisema huku 'akiwavunja mbavu' waombelezaji kutokana na maneno yake ya utani.

Alitaja mambo makubwa yaliyofanywa na Hayati Dk. Magufuli katika uongozi wake, kuwa ni pamoja na kutekeleza maagizo ya Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere ya serikali kuhamia Dodoma na mengine mengi yenye maslahi kwa Tanzania.

Rais mstaafu wa awamu ya saba Zanzibar, Dk. Ali Mohammed Shein, alisema sifa kubwa ya Rais Magufuli ilikuwa ni mkweli wa dhati, muungwana na hakuogopa binadamu mwenzake, bali Mungu.

"Ni mtu ambaye anadhibiti siri anayosema na kuyafanya hamkaripii asiyehusika, wengi wanasema mkali, siyo mkali, ni kiongozi na ni lazima aongoze kwa misingi ya haki na usawa, ameyafanya haya kwa vitendo, wengi wetu tumeyaona, tumeshuhudia, alikuwa anaona mbali zaidi," alisema.

# Mabeyo: Nilipewa ujumbe na JPM

**Na Romana Mallya**

MKUU wa Majeshi ya Ulinzi, Jenerali Venance Mabeyo, amesema Rais John Magufuli alimpa ujumbe maalum kabla hajafikwa na umauti.

Hata hivyo, kiongozi huyo wa kijeshi amesema hawezi kuuweka wazi ujumbe huo, bali atauwasilisha kwa Rais Samia Suluhu Hassan.

Jenerali Mabeyo alitoa kauli hiyo jana wilayani Chato mkoani Geita alipowasilisha salamu za rambirambi za vyombo vya ulinzi na usalama kufuatia kifo cha Rais John Magufuli, wakati wa misa ya maziko ya kiongozi huyo.

Alisema kuwa Rais Magufuli alimdokeza kitu ambacho angependa kukieleza kwa kiongozi mpya wa nchi, hivyo akamwomba Rais Samia ampe nafasi ya kumwona na kupokea ujumbe huo.

"Binafsi alinidokeza, lakini ninaomba nisitoe dokezo hilo hapa, ninaomba nije nikuone ofisini," Jenerali Mabeyo alisema.

Vilevile, Jenerali Mabeyo alimhakikishia Rais Samia kuwa vyombo vyote vya ulinzi na usalama, vitaendelea kumlinda na kumtii kama Amiri Jeshi Mkuu.



Akitoa salamu hizo kabla ya maziko yaliyofanyika jana jioni, Jenerali Mabeyo alisema: "Vyombo vya ulinzi na usalama vinakuhakikishia kuwa ulinzi wa nchi na mipaka yake ni salama na vitaendelea kukulinda wewe kama Rais, kukutii kama Amiri Jeshi Mkuu ili kutekeleza majukumu yako kama ilivyoainishwa kwenye Katiba," alisema.

Alimweleza Rais kuwa vyombo vya ulinzi na usalama vinamhakikishia utiifu, uadilifu na uaminifu mkubwa kwake Amiri Jeshi Mkuu kama ilivyo mila na desturi za majeshi katika awamu zote zilizopita za uongozi kwa manufaa ya ulinzi, usalama na ujenzi wa taifa.

Jenerali Mabeyo alisema vyombo hivyo vinampongeza kwa dhati kwa kuapishwa kwake kuwa Rais wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu kwa mujibu wa Katiba na kubainisha kwamba hali ilivyo sasa nchini ni tulivu na mipaka yote iko salama.

Kuhusu kifo cha Rais Magufuli, Jenerali Mabeyo alisema walikipokea kwa masikitiko na mshtuko mkubwa kwa kuwa wengi hawakutarajia.

Alisema baada ya ziara ya Rais Magufuli ya uwekaji wa jiwe la msingi kwenye kiwanda cha ushonaji Bohari Kuu ya Jeshi la Polisi na kufungua majengo ya Chuo cha Taaluma ya Polisi Kurasini, Dar es Salaam, alipanga Machi 10, mwaka huu kuwatunuku kamisheni maofisa wanafunzi wa Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania Ikulu ya Chamwino, Dodoma.

Alisema wanafunzi hao walikuwa wameshahitimu mafunzo yao na kwa mara ya kwanza walikuwa watunukiwe Februari 20, mwaka huu, lakini kutokana na ziara hiyo, alisogeza mbele hadi Machi 6.

"Alipokuwa Dar es Salaam, alipomaliza ziara Jeshi la Polisi, aliniambia hajisikii vizuri na akaniambia ninaonaje tusogeze hadi Machi 10, atazamie hali yake, lakini bahati mbaya haikuwezekana kutokana na maradhi hayo," alisema.

Jenerali Mabeyo alisema kwa kuwa wanafunzi wapo tayari, Rais Samia anakaribishwa kwa mara ya kwanza kutoa kamisheni kwa maofisa hao kwa tarehe atakayoona inafaa.

Alisema Rais Magufuli tangu aingie madarakani mwaka 2015, alionyesha kuviamini vyombo vya ulinzi na usalama, akiviwezesha kwa mahitaji ya kiutendaji na kiutawala ili vitekeleze majukumu yake ya kiulinzi na usalama kwa ufanisi.

Spika wa Bunge, Job Ndugai, alisema Bunge linamhakikishia Rais Samia kuwa litasimama naye kwa kila wanaloweza kufanya, afanikiwe pamoja na nchi.

"Ninamkaribisha bungeni, pale ndipo anaweza kuzungumza na Watanzania wote kwa hotuba, tunaomba aipange kwa siku atakayoona inafaa.

"Ninaomba niwaachie neno, Isaya 41:10, tunaambiwa tusiogope kwa vile yeye Mungu yu pamoja nasi. Mungu anatuambia tusifadhaike kwa vile Mungu wetu atatutia nguvu, nami nitawasaidia, nitawashika kwa mkono wangu wa kuume, hakika Bwana hatatuacha! Amina," alisema.

Jaji Mkuu wa Tanzania, Prof. Ibrahim Hamis Juma, alisema kuwa Januari 17 mwaka 2017, Rais Magufuli alimteua kuwa Kaimu Jaji Mkuu na Novemba 10, mwaka huo alimteua kuwa Jaji Mkuu.

"Tulipokuja kuzindua Mahakama ya Wilaya ya Chato, alitokwa machozi baada ya kusikia wimbo wa kwaya kuhusu hali ya umaskini, alipenda kujiita jiwe lakini kuna mambo yalifanya jiwe litoe machozi.

"Historia yake itaendelea kujiandika, nimepokea salamu za rambirambi kutoka kwa majaji wakuu wa Bara la Afrika, majaji wamemzungumzia Rais Magufuli kama kiongozi mwenye maono ya mbali aliyetumia uwezo wake wote kustawisha na kutetea maslahi ya Tanzania na Afrika kwa dhati," alisema.

Jaji Mkuu alisema Rais Magufuli alikuwa sauti mbadala kwa sababu alikuwa anaongea mambo ambayo wengine walikuwa hawataki kuyaongea.

"Alikuwa kiongozi ambaye alikuwa anahoji, anahoji karne 21 ambayo ni karne ya ushindani, alihoji sheria zetu, taratibu zetu, kwamba hazina kazi inayokwenda na matarajio ya karne ya 21, alihoji kila kitu," alisema.

# Wachambuzi waeleza matarajio kwa Samia

**Na Maulid Mmbaga**

BAADHI ya wachambuzi wa masuala ya kisiasa na wakazi wa Dar es Salaam wameeleza matarajio yao kwa uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan katika ustawi wa demokrasia na maendeleo ya taifa kwa ujumla.

Mmoja wa wachambuzi hao, Said Miraji, alisema ustawi wa demokrasia nchini utachangia maendeleo kwa kuwa watu watakuwa na uhuru wa kutoa mawazo na kushiriki katika masuala mbalimbali na hata kukosoa pale patakapokuwa panakosewa.

"Kila jambo lina faida na hasara lakini serikali ikifungua milango ya kidemokrasia na viongozi wakasimamia vizuri, faida itakuwa kubwa zaidi kuliko hasara na watu watakuwa na mapenzi baina yao," alisema.

Abdukarim Atiki, ambaye pia ni mchambuzi wa masuala ya kisiasa, alisema aliyekuwa Hayati Rais John Magufuli alipinga utaratibu wa walionacho kuwanyonya wasionacho.

Alisema si Tanzania tu ambayo inapingana kisiasa na aliziorodhesha nchi zingine zinazotumia mfumo huo zikiwamo Venezuela na Quba na kwamba msimamo huo uliazishwa na Rais wa Kwanza wa Tanzania, Hayati Mwalimu Julius Nyerere katika kudai kilicho chao uendelezwe.

"Huo ndio msimamo aliotuachia Mwalimu Nyerere kwamba ni lazima utu na heshima ya mwanadamu kiwe mstari wa mbele kwa ajili ya Watanzania na maslahi ya taifa kwa ujumla," alisema.

Batuli Adam, mkazi wa Dar es Salaam, alisema Watanzania katika kipindi hiki wanatakiwa kushikamana na kuwa na ushirikiano katika kuhakikisha taifa linaendelea kutoka pale Hayati Magufuli alipoishia.

"Tuna matumaini na Rais Samia katika kutuongoza na kutusimamia vizuri Watanzania na kutokana na umahiri wake katika utendaji atatuletea maendeleo zaidi katika taifa letu," alisema.

Naye Hamza Juma alisema kwa wakati huu serikali inapaswa kukaa pamoja na waiangalie katiba na kutafakari mwanzo mpya wa kuanza nao ili uweze kuwasaidia wao na wananchi kwa ujumla.

"Rais Samia atumie vizuri katiba pamoja na viongozi walio chini yake katika kutekeleza majukumu yake na tuna imani atayatekeleza majukumu yake kwa weledi wa hali ya juu kwa kuwa alishapata uzoefu kutoka kwa Rais Magufuli enzi za uongozi wake akiwa Makamu wa Rais," alisema.

# DC azuia vibali vya muziki

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

MKUU wa Wilaya ya Wanging'ombe mkoani Njombe, Lauteri Kanoni (pichani), amewataka wananchi kupunguza ulevi huku akizuia kutolewa kwa vibali vya matamasha ya burudani katika kipindi cha maombolezo ya kifo cha Rais John Magufuli.

Marufuku hiyo aliitangaza jana akiwa katika Kata ya Igwachanya wakati wa mkutano wa maombolezo ya msiba huo wa kitaifa.

Alisema kitendo cha kufanya matamasha ya burudani na ulevi wa kupindukia havitavumiliwa katika kipindi chote cha siku 21 za maombolezo ya msiba huo.

"Itatushangaza sana, tunalia kilio kikubwa hivi halafu watu kwenye baa wanapiga 'ndomboloo ya solo', ina maana wewe hauko pamoja na sisi.



"Ninaelekeza tupige nyimbo za maombolezo na tupunguze ulevi. Hakuna vibali vya 'disco' vitakavyotolewa kwa kipindi hiki, tutakuwa tumekiuka taratibu," aliagiza.

Awali, Katibu Tawala wa Wilaya ya Wanging'ombe, Edward Manga, alisema mchango wa Rais Magufuli katika taifa umekuwa wa kuigwa barani Afrika kwa kuwa amefanikiwa kuifikisha nchi katika uchumi wa kati kabla ya wakati uliopangwa.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Wanging'ombe, Agnetha Mpangile, alisema pigo lililowakuta Watanzania la kuondokewa na Rais Magufuli halitosahaulika.

Viongozi wa dini, akiwamo Mbaraka Thabiti, Sheikh wa wilaya hiyo, walisema Watanzania hatupaswi kukata tamaa kwa kuwa maandiko yanasema baada ya kifo cha Mussa, alitumwa Joshua kwenda kuwafikisha wana wa Israel kwenye nchi ya ahadi.

"Baadhi ya wakazi wa Wanging'ombe, wakiwamo Aiden Valanzi na Erasto Homange, walisema kifo cha Rais Magufuli kimewagusa kwa kuwa aliwatetea wanyonge.




Baadhi ya wakazi wa Jiji la Arusha, wakifuatilia ibada ya maziko ya aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. John Magufuli, kupitia luninga zilizofungwa nje ya Ofisi za Chama Cha Mapinduzi (CCM), mkoa jana. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

# Watumishi madini wapewa kibano

**Na Beatrice Shayo**

MKUU wa Wilaya ya Bariadi, Festo Kiswaga, amepiga marufuku watumishi wa idara ya madini kwenda kusimamia na kukusanya mirahaba na kodi zote za serikali katika Mgodi wa Bulumbaka Gasuma.

Kiswaga amesema badala yake mgodi huo utasimamiwa na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya hiyo.

Alitoa agizo hilo juzi wakati akizungumza na wachimbaji wadogo wa mgodini huo na kubainisha kuwa watumishi hao wamepewa kazi hizo kinyemela na Kaimu Ofisa wa Madini Mkoa wa Simiyu, Joseph Kumburu.

"Alikuwa naye mtu huyu Kahama huko katika mgodi unaitwa Wime, amemleta akusanye mapato hapa, kwa nini? Na huyo mtu ninayemsema, amepewa kazi kisheria kusimamia Dutwa Two pale, haitoshi amemleta hapa Bulumbaka kinyemela," alisema Kiswaga.

"Kwa mujibu wa sheria, kama anataka kumleta mtu yeyote hapa, alitakiwa ashirikiane na maofisa wa kutoka Kamati ya Ulinzi na Usalama.

"Kwa akili ya kawaida, hivi kweli mhasibu atoke Kahama, Simiyu yote hii haina mhasibu na Bariadi yote haina mhasibu, Bulumbaka hii hakuna mpaka rafiki yake atoke Kahama?" alihoji Kiswaga.

Alisema mgodi huo siyo mali ya familia, hivyo alimwagiza Mkuu wa Polisi Wilaya ya Bariadi kuwakamata watu hao watakapoonekana mgodini huko wakikusanya mapato ya serikali.

"OCD hao watu wakionekana hapa, kamata weka ndani," aliagiza Kiswaga huku wachimbaji wadogo wakishangilia.

Kaimu Ofisa Madini Mkoa wa Simiyu, Joseph Kumbaru, alisema hana cha kuzungumza kwa sababu hakuwa na taarifa za Mkuu wa Wilaya huyo kwenda katika mgodi huo.

"Kwa sasa siwezi kusema chochote kuhusu suala hilo, binafsi sina taarifa ya huyo Mkuu wa Wilaya, hivyo ninaomba unipe muda tutazungumza wakati mwingine," alisema.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Taifa Stars bado ina nafasi kumuenzi vyema Magufuli

**BAADA** ya kukamilisha taratibu za kumzika aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. John Pombe Magufuli huko nyumbani kwao Chato mkoani Geita jana, Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), bado ina nafasi ya kumuenzi vyema kiongozi huyo.

Taifa Stars ambayo juzi ilikubali kichapo cha bao 1-0 kutoka kwa wenyeji Equatorial Guinea na kupoteza nafasi ya kushiriki katika fainali zijazo za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON), kutokana na kuvuna pointi nne katika mechi tano ilizocheza.

Tunisia iliyofikisha pointi 13 na Equatorial Guinea ambayo juzi usiku ilifikisha pointi tisa, ndio zimefuzu kushiriki fainali hizo kutoka katika Kundi J ambapo Tanzania (Taifa Stars) yenye pointi nne, na Libya inayoburuza mkia ikiwa na pointi tatu baada ya kucheza mechi tano, zitabakia kuwa watazamaji kwenye michuano hiyo itakayochezwa baadaye nchini Cameroon.

Ili kumuenzi vyema Rais Magufuli, Taifa Stars itatakiwa kumaliza mechi ya hatua ya makundi dhidi ya Libya ambayo itachezwa kesho Jumapili kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

Ingawa mechi hiyo haitaipeleka kokote Taifa Stars ambayo sasa hivi inafundishwa na Kocha Mkuu, Kim Poulsen ambaye ni raia wa Denmark, lakini itatusaidia Watanzania kufuta machozi ya msiba huo mzito ambao umetokea katika nchi yetu.

Stars itatakiwa kucheza kufa na kupona na kuhakikisha inapata pointi tatu katika mechi hiyo itakayoonekana ya kukamilisha ratiba, lakini ushindi wake itaisaidia nchi kupanda katika viwango vinavyotolewa na Shirikisho la Soka la Kimataifa (Fifa).

Wachezaji watakaopata nafasi ya kucheza katika mechi hiyo watatakiwa kujituma na kupambana wakati wote ili kupata matokeo mazuri kwa sababu itawasaidia kuwatangaza kupitia mawakala mbalimbali ambao wanafuatilia michuano hiyo kwa kuwatafutia masoko kwenye timu za mataifa ya Ulaya.

Pia mechi hiyo itakuwa ni sehemu ya maandalizi kuelekea mechi za kufuzu kucheza Fainali za Kombe la Dunia ambapo timu hiyo bado ina kibarua kizito cha kukata tiketi ya kushiriki mashindano hayo kwa mara ya kwanza.

Nipashe inaamini endapo Taifa Stars itafanikiwa kukata tiketi ya kushiriki Fainali za Kombe la Dunia kwa mara ya kwanza, itakuwa ni zawadi nzuri kwa Rais Magufuli ambaye siku zote alikuwa anasisitiza anapenda kuona timu za Tanzania zinashinda.

Kuteleza si kuanguka, Taifa Stars huu ni wakati ya kujipanga upya na kuhakikisha ndoto za Tanzania kushiriki mashindano makubwa zinatimia na itapendeza kama hili litafanikiwa wakati huu bado machungu ya msiba hayajasahaulika.


Kama mwaka juzi timu hiyo ilipambana na kuhakikisha inashiriki fainali za AFCON zilizofanyika nchini Misri, basi kwa nguvu ile ile au zaidi wachezaji wanatakiwa wajitume na kuwafuta machi Watanzania kwa kukata tiketi ya kucheza mashindano ya Kombe la Dunia kwa mara ya kwanza.

Hakuna kisichowezekana, kama mipango madhubuti ilifanyika na kuifanya Stars kucheza AFCON kwa mara ya pili baada ya miaka 39 kupita, pia inawezekana mikakati ikaimarishwa na timu hiyo ikakata tiketi ya kushiriki Kombe la Dunia huko Qatar mwakani.

Mungu ibariki Taifa Stars, Mungu ibariki Tanzania, Pumzika kwa amani Rais Magufuli.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Ujinga wa kuuza si ubaradhuli...

Na Barnabas Maro

**HAKIKA** ujinga wa kuuza si ubaradhuli wa kununua. Kwa muktadha huu, maana ya "ubaradhuli"ni tabia ya kukosa adabu na heshima hali ya kujifanya mjuaji au mjanja na hasa kwa kuwa na nia mbaya.

Ndio maana wahenga walisema "Ujinga wa kuuza si ubaradhuli wa kununua" yaani ni heri kuwa mjinga wa kununua.

Methali hii hutumika kuwakumbusha watu umuhimu wa kuwa makini na tahadhari wanunuapo au wanapopendekezewa kitu fulani.

Leo nazungumzia mambo yanayofanywa na baadhi ya mashabiki wa Yanga na Simba wanaozishabikia timu ngeni za ughaibuni zinapocheza kandanda na timu hizo za Dar es Salaam eti ziitwazo "watani wa jadi!"

Usahihi wa maana ya neno "utani" ni maneno au vitendo vya dhihaka; mzaha. Tabia ya watu kufanyiana masihara kwa lengo la kuambiana ukweli na kuimarisha uhusiano wao. Kwa hiyo ni dhahiri ya kuwa watani ni watu wanaoshirikiana na kusaidiana wakati mmoja anapokuwa kwenye matatizo.

Kwa upande mwingine, husemwa: "Ukiwa na lako usitazame la wenzio." Maana yake kama una jambo lako la kufanya usiliingilie la mwenzako. Hutumiwa kutambulisha umuhimu wa kufanya mambo tunayowajibika kufanya badala ya kujihusisha na watu wengine.

Timu za Simba na Namungo zinaiwakilisha Tanzania kwenye michezo ya kimataifa hapa barani Afrika. Timu hizo zikishinda huwa ni fahari yaani jambo au kitu bora cha kujivunia kwa watu. Kwa muktadha huu ni sifa kwa Tanzania na sio vilabu husika yaani Simba na Namungo.

Ni bahati mbaya sana kuwa baadhi ya mashabiki wa Yanga na Simba wanaweka kando umuhimu wa kuzitetea timu zao zinapopambana na timu ngeni kutoka nje ya Tanzania!

Yanga ichezapo na timu ngeni kutoka nje ya Tanzania, baadhi ya mashabiki wa Simba huzishangilia timu ngeni kwa bidii na hoihoi, yaani sauti ya furaha, shangwe na nderemo za kusherehekea; chereko, vifijo! Ujinga huo hufanywa pia na mashabiki wa Yanga, Simba inaposhindana na timu ngeni!

Ujinga ni hali ya kukosa; ubozi, ubwege. Ndio maana wahenga walisema: "Wajinga ndio waliwao." Maana yake wajinga ndio wanaopumbazwa au kuliwa. Methali hii huweza kutumiwa kumpigia mfano mtu ambaye ameishia kudanganywa kwa njia inayoonekana kuwa rahisi sana.

Eti mashabiki wa Yanga na Simba huzishangilia sana timu za ughaibuni zinapocheza na mojawapo ya timu hizo (Yanga au Simba) na kuizomea mojawapo inayoshindwa! Je, hawatambui umuhimu wa nchi yao au ni kuoneana gere yaani choyo inayotokana na husuda? Watu wa nchi moja ni ndugu lakini kwa Yanga na Simba ni maadui!

Kwa sababu hiyo timu ngeni zinapokuja nchini kupambana na timu hizo huwa hazina wasiwasi kwani zinajua zitapata washangiliaji wa Tanzania; na huwa hivyo!

Ndo maana wahenga walisema: " Salala huvunja jiwe, kaifa mwanadamu." Salala ni neno linaloonesha hisia ya kushangaa. Maana yake kama laana au apizo huvunja jiwe seuze kwa binadamu?

Hii ni methali ya kutumiwa kumkumbusha mtu madhara yanayoweza kutokana na kusemwa vibaya na watu wengine. Hutushauri tutahadhari na kutiwa vinywani na watu kwa ubaya kwani tunaweza kupatwa na mabaya.

Tunapaswa kutambua kwamba Simba na Namungo zikishinda mechi zao dhidi ya timu za nchi zingine, sifa itakuwa kwa Tanzania kwanza kwani zitakuwa zimeitendea haki bendera ya Taifa letu kwanza na bendera za vilabu zinafuata.

Kinyume chake nchi za nje zitatuona kama watu tusio na akili; wapumbavu, punguani. Kwa nini tunajidhalilisha wenyewe? Kwa nini watu wa nchi moja, tuwe na upasi yaani hali ya kutopendana, kisa gozi la ng'ombe nyama kala nani? Aibu iliyoje!

"Ndugu mui afadhali kuwa naye." Ni afadhali kuwa na ndugu yako hata kama ni m-baya. Methali hii hutumika kutunasihi tuwathamini ndugu zetu hata kama wana sifa mbaya kiasi gani. Nduguyo aweza kukufanyia hisani ambayo rafiki hawezi.

***marobarnabas@yahoo.com***
***0784 334 096***



Waziri Mkuu Kassim Majaliwa na mkewe Mary Majaliwa, wakiweka shada la maua.



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Mwinyi na mkewe Mariam Mwinyi, wakiweka shada la maua kwenye kaburi la Hayati Dk. John Magufuli, baada ya maziko yaliyofanyika nyumbani kwake, Kijiji cha Mlimani, Chato, mkoani Geita jana. **PICHA ZOTE: MAELEZO**



Spika Job Ndugai na mkewe Dk. Fatma Mganga, wakiweka shada la maua.



Sheikh Mkuu wa Tanzania, Mufti Abubakar Zubeir, akiweka shada la maua.



Rais wa Baraza la Maaskofu Tanzania (TEC), Askofu Mkuu Gervas Nyaisonga, akiweka shada la maua.



Sehemu ya mawaziri waliohudhuria maziko ya Hayati Dk. John Magufuli.

# Watanzania wasisitizwa kutumia 'Tiketi Mtandao'

**Na Joseph Mwendapole**

WATANZANIA wametakiwa kuchangamkia mfumo mpya wa 'Tiketi Mtandao' kukata tiketi za mabasi kwa kutumia simu zao za mkononi ili kuondoa gharama za kusafiri kwenda kwenye vituo vya mabasi.

Wito huo ulitolewa jana na Kaimu Katibu Mtendaji wa Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma Usafiri Ardhini (LATRA-CCC), Leo Ngowi, wakati akizungumzia mfumo huo.

Alisema mfumo huo ni mkombozi si tu kwa wenye mabasi bali na wananchi ambao walikuwa wakilazimika kusafiri umbali mrefu kwenda kukata tiketi za mabasi. Alisema hata abiria ambao hawana simu janja wanaweza kupata tiketi mtandao kwa kwenda kwenye vituo vya mabasi au kutumia simu za jamaa zao badala ya kusafiri hadi kwenye vituo vya mabasi.

Ngowi alisema kutokana na umuhimu wa mfumo huo mpya, LATRA-CCC imekuwa ikitoa elimu endelevu kuhusu matumizi ya mfumo huo mpya ili kuwawezesha Watanzania wengi kuujua na kuanza kuutumia.

Alisema hadi sasa wameshawafikia zaidi ya abiria 100 ambao wamewafundisha na baada ya kujua kuutumia, wameupongeza kuwa unawarahishia safari za mara kwa mara kwenda kukata tiketi.

"Kwanza ni rahisi sana mtu anakwenda 'Play Store' kwenye simu yake kisha anapakua 'app' ya tiketi mtandao ambayo ataikuta na kisha anafuata maelekezo mpaka anakatiwa tiketi yake na LATRA-CCC. Tunaamini iwapo nusu tu ya Watanzania watautumia utakuwa na manufaa makubwa kwenye uchumi wetu kwasababu kuna fedha zilikuwa zinapotea tu," alisema Ngowi.

Alisema baraza limeweka utaratibu endelevu wa kufika kwenye stendi ya mabasi Mbezi, Dar es Salaam na kukutana na abiria kwaajili ya kuwaelimisha kuhusu matumizi ya mfumo huo mpya wa kukata tiketi.

Ngowi alisema uzuri wa mfumo huo ni kwamba mtu yeyote anaweza kufanyiwa wekesho (booking) na kukatiwa tiketi na mtu mwingine akiwa sehemu yoyote hapa nchini.

Kupitia mfumo huo mpya uliozinduliwa hivi karibuni na Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA), msafiri anaweza kukata tiketi kwa kutumia simu yake au mashine maalum ya kukatia tiketi POS.



Muuza nyama ya kuku akifanya biashara yake jirani na dampo la takataka katika Soko la Mabibo karibu na Chuo cha Usafirishaji (NIT), Manispaa ya Ubungo, mkoani Dar es Salaam jana, kitendo ambacho ni hatari kwa afya ya walaji.
**PICHA: MIRAJI MSALA**

# Maambukizi TB Njombe yapaa

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

ZAIDI ya watu 300 huambukizwa kifua kikuu (TB) kwa mwaka katika Halmashauri ya Mji wa Njombe huku Tanzania ikiwa ni zaidi ya watu 64,000 sawa na wagonjwa 176 kila siku kwa takwimu za mwaka 2011 hadi 2017.

Hayo yalibainishwa juzi na Mratibu wa Kifua Kikuu wa Halmashauri ya Mji wa Njombe, Dk. Kisulila Matanga, kwa niaba ya mganga mkuu wa halmashauri wakati akitoa semina kwa waandishi wa habari pamoja na kufuatilia mafunzo kwa wauzaji wa maduka muhimu ya binadamu yaliyofanyika mjini humo.

Dk. Kisulila alitumia nafasi hiyo kumshukuru Hayati Dk. John Magufuli aliyekuwa Rais wa awamu ya tano kwa ujenzi wa hospitali na vituo vya afya na kuongeza vifaa mbalimbali vikiwamo vya kutambua tatizo hilo na kutibu ili kupunguza ongezeko la waathirika wa kifua kikuu nchini.

Alisema ugonjwa wa kifua kikuu umegawanyika katika madaraja mawili huku ugonjwa huo ukitibiwa bure nchini kutokana na juhudi mbalimbali zilizofanywa na serikali.

"Kuna madaraja mawili ya kifua kikuu. Moja ni kifua kikuu lakini pia na kifua kikuu sugu ambacho kinahitaji matibabu ambayo yako tofauti na matibabu ya kifua kikuu cha kawaida na wakati mwingine mgonjwa wa kifua kikuu anaingia mpaka gharama lakini ikumbukwe matibabu ya kifua kikuu ni bure," alisema Dk. Kisulila.

Hata hivyo alitaja makundi ya watu wanaoweza kupata maambukizi ya kifua kikuu likiwamo kundi la watu wanaokuwa kwenye eneo lenye giza kwa muda mrefu kama kuishi katika nyumba yenye madirisha madogo.

"Kwanza ni watu wanaokunywa pombe kwa wingi, wenye magonjwa ya muda mrefu ikiwamo saratani na sukari lakini kundi lingine ni la wagonjwa wanaoishi na maambukizi ya virusi vya UKimwi (VVU), wachimbaji wa madini na wale walio kwenye miingiliano mikubwa," alisema.

# TBS yashauri kumuezi JPM kwa kupiga vita bidhaa hafifu

**Na Mwandishi Wetu**

SHIRIKA la Viwango Tanzania (TBS) limewataka wananchi kushiriki katika vita ya kutokomeza bidhaa hafifu nchini ikiwa ni sehemu ya kumuenzi aliyekuwa Rais wa Tanzania, John Magufuli katika ujenzi wa Tanzania ya viwanda.

Kauli hiyo ilitolewa kwa nyakati tofauti na Ofisa Masoko wa TBS, Deborah Haule, wakati wa kuhitimisha kampeni ya kutoa elimu kwa umma katika wilaya za Musoma, Chato na Karagwe kuhusu umuhimu wa kununua bidhaa zilizothibitishwa na shirika hilo sambamba na kuwahamasisha wafanyabiashara kusajili maduka ya chakula na vipodozi.

Alisema Hayati Dk. Magufuli aliamini katika kukuza uchumi kupitia viwanda na TBS inaahidi kuyaishi maono yake kwa kuhakikisha wanaendelea na juhudi za kuvisaidia viwanda kuzalisha bidhaa bora.

Haule alisema uwapo wa bidhaa bora na zenye viwango utawezesha kukubalika ndani na nje ya nchi kirahisi na hasa zile za wajasiriamali wadogo kwa kuwa ndicho kilikuwa kilio chake kikubwa kwa hawa wadogo kuingiza bidhaa zao katika masoko ya nje.

"Haya yatawezekana kwa kutoa elimu ya ubora kwa umma na mafunzo ya viwango kwa wazalishaji wadogo sambamba na kuwalea mpaka kukuua na kujisimamia katika masuala ya ubora chini ya mpango wetu wa kusaidia wajasiriamali wadogo," alisema.

Kampeni hiyo ya elimu kwa umma ilifanyika katika maeneo mbalimbali yakiwamo ya shule za msingi na sekondari, masoko, stendi, minadani na maeneo mengine ya wazi ambapo wananchi walijitokeza kupata elimu na ufahamu wa masuala mbalimbali yahusuyo ubora wa bidhaa.

Mkurugenzi wa Halmashauri Manispaa ya Musoma, Fidelica Myovella, aliipongeza TBS kwa kutoa elimu kwa wananchi katika ngazi ya wilaya kwani itaongeza ufahamu na kuhakikisha suala la uuzaji wa bidhaa hafifu sokoni linapungua kama sio kwisha kabisa.

Haule aliwakumbusha wananchi wote kuwa vita ya bidhaa hafifu sio ya TBS pekee bali ni ya taifa kwa ujumla.

"Kampeni hii imewafikia wananchi 14,517 kati yao wanafunzi wa shule za Msingi na Sekondari 12,204 na wananchi 2,313," alisema Haule.

Haule aliwafafanulia wanafunzi pamoja na walimu umuhimu wa viwango katika maisha yao ya kila siku vile vile kuwafahamisha fursa ya huduma bure kwa wajasiriamali wadogo.

Hata hivyo, aliwaasa wawe mabalozi wazuri wa kuhamasisha ubora katika jamii wanazoishi.

Vilevile aliwasisitiza wananchi kuendelea kutoa taarifa pindi wanapokutana na bidhaa zilizokwisha muda wake au wanapotilia shaka bidhaa yoyote katika soko na wafanyabiashara kufuatilia taratibu sahihi za usajili wa bidhaa au majengo kupitia mawasiliano waliyopewa.

Diwani wa Kata ya Bugene wilayani Karagwe, Mugisha Mathias, aliipongeza TBS kwa elimu ambayo wanaitoa katika wilaya hiyo kwani kuna baadhi ya wafanyabiashara na wananchi kwa ujumla hawakuwa na elimu ya ubora wa bidhaa kwa undani zaidi.



# Malecela aeleza namna ya kumuenzi JPM

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

WAZIRI Mkuu Mstaafu, John Malecela, amesema namna nzuri ya kumuenzi Hayati Rais John Magufuli ni kukamilisha miradi aliyoanzisha.

Akizungumza hivi karibuni kuhusu kifo cha Rais Magufuli, Malecela alisema wakati wa uongozi wake ametekeleza miradi mikubwa na mingine bado haijakamilika, hivyo ni vyema akaenziwa kwa kukamilisha kuitekeleza.

"Kuna ujenzi wa reli ya kisasa, bwawa la Nyerere kwa ajili ya kuzalisha umeme. Ni mtu aliyefanya mambo makubwa ambayo watu hawakutegemea, yale ambayo ametuyaachia tukitekeleza na kuyamaliza tutafika mbali, tutekeleze reli ya umeme kutoka Dar es Salaam hadi Mwanza,"alisema.

Kuhusu matumaini kwa Rais Samia Hassan Suluhu, kiongozi huyo alisema ni jambo la kushukuru Mungu kwa kuwa Tanzania haina ubaguzi wa kijinsia.

"Sisi mtawala ni mtawala, namtakia kila la heri. Sisi tutakuwa tumetekeleza wazo la Watanzania la kusema sisi hatujali jinsia sisi tunajali mtu anayetumikia nchi yake, Samia ameonyesha uwezo wa hali ya juu kwa kuwa ni mtu aliyefanya kazi na Magufuli kwa kasi lazima mtu anakuwa na uwezo mkubwa," alisema Malecela.

Kuhusu uimara wa CCM, Malecela alisema Hayati Magufuli aliahidi kukiacha chama kikiwa na nguvu na alifanya kazi na kukiacha chama kikiwa na nguvu. "Nguvu imeonekana katika uchaguzi uliopita, baada ya kuonyesha nguvu ile, mafisadi wowote watakaokuja kujaribu kuleta mfarakano katika CCM tutawashughulikia na hatutawaruhusu kamwe kujaribu kukigawa chama," alisema.

Alitoa wito kwa Watanzania kuendelea kuifanya Tanzania kuwa na mshikamano wa hali ya juu na kuifanya kuwa nchi ya mshikamano na inayotaka maendeleo endelevu yanayoletwa na wananchi na viongozi wao.

"Mshikamano ambao utawainua wananchi kutoka kwenye hali ya umaskini, tuendelee kujivunia Tanzania," alisema.



Meneja wa Kanda ya Afrika Mashariki wa miradi ya Leonard Cheshire kutoka nchini Uganda, Catherine Alejo, akizungumza na wadau wa elimu kwenye mkutano wa kuhitimisha mradi wa elimu jumuishi, jijini Dodoma juzi. Kutoka kushoto ni Mshauri wa Elimu Jumuishi Mkoa wa Dodoma, Mtinduli Mwalonmgwe, Mkurugenzi wa Elimu Maalum (TAMISEMI), Migeha Julius na Mwenyekiti wa Bodi ya Taasisi ya Cheshire Tanzania, Mzee Masangia. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Wenye ulemavu 80 wasajiliwa elimu jumuishi

**Na Peter Mkwavila DODOMA**

SERIKALI imesema zaidi ya watoto 80 wenye ulemavu, wametambuliwa na kusajiliwa katika mfumo rasmi wa elimu jumuishi kupitia taasisi ya Tanzania Cheshire Foundation kwa kushirikiana na Leonard Cheshire.

Mkurugenzi wa Elimu Maalum kutoka Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Julius Migeha, aliyasema hayo alipokuwa akizungumza na wadau mbalimbali wa elimu wakiwamo wazazi na walezi wenye watoto ambao wana ulemavu katika mkutano wa kuhitimisha mradi wa elimu jumuishi uliofanyika jijini hapa.

Alisema taasisi hiyo imetoa elimu ya mafunzo kazini kwa zaidi ya walimu 200 kuhusu ufanikishaji na uendeshaji wa madarasa jumuishi.

"Miradi hii mingine ambayo imefanyika na taasisi hii ni kujenga na kukarabati miundombinu ya shule ili iwe rafiki kwa watoto na kununua visaidizi kwa ajili ya wanafunzi, ununuzi wa vifaa mbalimbali vya kufundishia na kujifunzia na kuihamasisha jamii kuwabaini watoto wenye ulemavu na kuhimiza uandikishwaji shuleni," alisema.

Migeha alisema kuwa serikali itaendelea kuimarisha mifumo sahihi ya utoaji wa elimu kwa wanafunzi wenye uhitaji maalumu na walimu wataalamu.

Pia alisema kufanya uchunguzi wa watoto kabla ya kuandikishwa ili waandikishwe kwenye shule sahihi na kupatiwa hatua stahiki.

"Serikali ya Tanzania inatambua jitihada stahiki zinazofanywa na mashirika yasiyo ya kiserikali katika kushirikiana utoaji wa elimu bora kwa Watanzania hii ni pamoja na utekelezaji wa mpango wa elimu jumuishi," alisema.

Meneja wa Kanda ya Afrika Mashariki wa Mradi wa Leonard Cheshire kutoka nchini Uganda, Catherine Alejo, alisema wamefanikisha kwa asilimia kubwa kuwafikia walengwa katika nchi za Afrika Mashariki, watoto wenye ulemavu na uhitaji maalumu kwa kuboresha mazingira ya mahitaji yanayohitaji yao kwa kupitia elimu jumuishi ikiwamo kukarabati na kujenga majengo mbalimbali ya shule na utoaji wa vifaa mbalimbali vya ufundishaji na visaidizi.

"Mradi huo umetoa elimu mbalimbali kwa walimu ili kutambua mbinu za ufundishaji wa watoto ambao ni walemavu na wale wenye mahitaji maalumu ikiwamo na wazazi katika kuona umuhimu wa kuwapeleka watoto wao mashuleni badala ya kuwaficha majumbani (nyumbani)," alisema.

"Pamoja na kusitishwa kwa mradi huu kwa hivi sasa lakini tuna kila sababu ya kujivunia kutokana na mafanikio makubwa ambayo yaliyowezesha mradi huo kwa nchi za afrika mashariki, kwa kushirikiana na serikali husika kwenye upande wa ukarabati wa majengo ya shule, ununuzi wa vifaa mbalimbali kwa ajili ya walengwa husika," alisema.

Alisema mpango huo wa mradi wa elimu jumuishi unaohitimishwa mwaka huu ulilenga kuwajumuisha watoto wote, vijana na watu wazima katika kubaini na kushughulikia tofauti za mahitaji yao ya kujifunzia kwa kila mwanafunzi wakiwamo wenye ulemavu.

## Waganga wa jadi kumuezi Magufuli

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

UMOJA wa Waganga na Wakunga wa Tiba Asili (UWAWATA), umesema utamuenzi Hayati Rais John Magufuli kutokana na kutoa nafasi kwao kupata elimu ya muda mfupi juu ya utoaji wa tiba hiyo.

Katibu Mkuu wa UWAWATA, Lucas Mlipu, akizungumza na Nipashe, alisema uamuzi wa Hayati Magufuli wa kuruhusu wao kupata elimu ya utoaji tiba hiyo ni kuonyesha jinsi gani anathamini kazi inayofanywa na wao.

Mlipu alisema kipindi cha nyuma tiba asili haikuwa inajulikana sana lakini Hayati Magufuli ameifanya kujulikana baada ya kuhimiza matumizi ya tiba mbadala ikiwamo kutoa nafasi ya kupata elimu juu ya utoaji wa tiba asili.

"UWAWATA tutaendelea kumkumbuka Hayati John Magufuli kwa mchango mkubwa kwa umoja wetu, nasi tutaendelea kuenzi mazuri aliyotuachia," alisema Mlipu.

Kutokana na hilo, alisema umoja wao utaendelea kufanya mazuri ambayo wamekuwa wakihimizwa na serikali kuhusiana na utoaji wa Tiba asili kwa jamii inayowazunguka.

Aliwataka Watanzania wote kuwa na subira katika kipindi hiki kigumu lakini kila mmoja kuenzi mambo mazuri ya maendeleo ambayo ameyafanya katika uongozi wake.

Alisema ili kuhakikisha wanatimiza ndoto za Magufuli zinatimia watafanya kazi ya kuwahamasisha waganga hao wote kupata elimu ili kuinua tiba asili nchini.

Hata hivyo, alisema watamuenzi Rais Magufuli kwa kufanya kazi kwa bidii ikiwamo kutekeleza yale yote aliyokuwa akiyaeleza ya kuwasaidia Watanzania kupata huduma za tiba asili.

Naye Mratibu wa Elimu ya Kuinua Tiba Asili nchini, Ally Maganyari, alisema Hayati Magufuli alikuwa ni kiongozi wa kwanza kuwataka watoa huduma ya tiba asili kupata elimu ya muda mfupi juu ya utoaji wa tiba hiyo.

Alisema suala hilo limechangia kwa kiasi kikubwa kuwa wawazi kwa kile wanachokifanya hususani utoaji wa huduma ya tiba asili. Maganyari alisema ili kuhakikisha wanamuenzi Magufuli na kutimiza yale mazuri aliyowaachia ikiwamo kuwahamasisha waganga hao wote kupata elimu ili kuinua tiba asili nchini.

Alisema wana mpango wa kuzungumza na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ili wataalamu wake wa tiba asili wawe wanatoa elimu hiyo kila mkoa badala ya ilivyo sasa inapatikana Dodoma pekee.





# Watoto shule Magufuli waahidi kufanya vizuri ili kumuenzi JPM

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WANAFUNZI wa Shule ya Sekondari ya Dk. John Pombe Magufuli, Zanzibar, wamesema kifo cha aliyekuwa Rais wa Tanzania Dk. John Pombe Magufuli, ni pigo kwao.

Hayati Magufuli aliyefariki dunia Machi 17, mwaka huu, alizikwa nyumbani kwao Mlimani, Chato mkoani Geita.

Wanafunzi hao walisema juzi kuwa njia pekee ya wao kumuenzi ni kufanya vizuri katika mitihani yao ya taifa.

Walisema Magufuli alikuwa akipenda wanafunzi wasome kwa bidii, hivyo ili kumuenzi na kumkumbuka, waliahidi kusoma kwa bidii na kupata matokeo mazuri katika mitihani yao.

"Ili tusilichafue jina la shule hii ambalo ni jina la aliyekuwa Rais wa Tanzania niwaombe wanafunzi wezangu kuja na ufaulu mzuri katika mitihani yetu ya kidato cha nne ili iwe ni miongoni mwa shule bora zitakazofanya vizuri," alisema Ibrahim Khatib Hassan, mmoja wa wanafunzi wa shule hiyo.


Alisema Magufuli alikuwa akipendelea zaidi masomo ya sayansi, hivyo atafanya vizuri katika masomo hayo ili taifa kuwa na watalamu wazuri hapo baadaye.

Naye mwanafunzi Husna Abdul-aziz Muhammed, alimwomba Rais wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan, kutekeleza ahadi zilizowekwa na Hayati Magufuli wakati wa uhai wake alipoweka jiwe la msingi shuleni hapo mwaka 2019 ikiwamo kufuatilia maendeleo ya shule hiyo.

"Tunamwomba Rais Samia aje kututembelea na kutupatia misaada ili kuimarisha viwango vya elimu kama alivyotuahidi Dk. Magufuli," alisema.

Mkuu wa Shule hiyo, Victor Clement, alisema kifo cha Dk. Magufuli pigo kwa taifa zima na si kwa shule hiyo pekee na kuahidi kuendelea kutoa elimu bora ili wanafunzi kufanya vizuri bila kuchafua jina la shule hiyo.

Pia aliwataka wanafunzi wa shule hiyo kujikita zaidi katika masomo yao ili kufanya vizuri katika mitihani yao na kulipa heshima jina la shule.a na tija zaidi sanjari na kurahisisha biashara ya mtandao.



Makamu wa Kwanza wa Rais Zanzibar, Othman Masoud Othman (kushoto) na Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar, Hemed Suleiman, wakiwa katika ibada ya mazishi ya Hayati Dk. John Magufuli, wilayani Chato, mkoani Geita jana. **PICHA: MAELEZO**

# Ataka usawa kijinsia kukomboa wanawake

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

OFISA Uwezeshaji Uchumi Wanawake kupitia Mradi wa Viungo Zanzibar (Spice), Nairat Abdalla Ali, amesema kukosekana kwa usawa wa kijinsia katika jamii, wanawake wengi wakiwamo watu wenye ulemavu wataendelea kukabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwamo za umiliki wa ardhi na hali duni kiuchumi.

Aliyasema hayo jana alipokuwa akizungumza na waandishi habari mjini Unguja wakati wakitoa mafunzo kwa wakulima mbalimbali kutoka wilaya ya Kusini Magharibi A pamoja na Wilaya ya Kati Unguja.

Nairat alisema wanawake wengi Zanzibar wamekuwa wakikosa haki za msingi kutokana vikwazo tofauti vikiwamo kutoshirikishwa katika shughuli mbalimbali za kimaendeleo jambo ambalo linaendelea kurudisha nyuma jitihada zao.

Kwa kuliona hilo, alisema kupitia mradi huo wa viungo wameona kuna haja kutoa elimu ya jinsia kwa wakulima hao na elimu hiyo itabadili mtazamo hasi na hatimaye wanawake wengi kupewa fursa.

"Tunaamini kuwa elimu hii itawazindua wanaume hawa na wanawake walioshiriki na watakaoendelea kushiriki hatimaye kupata mabadiliko makubwa," alisema.

Pia alisema ili jamii ipige hatua zaidi kimaendeleo, hakuna budi kuwapo kwa usawa wa kijinsia bila ya ubaguzi wa haki kwa wanaume na wanawake.

Mtalamu wa maswala ya kijinsia kutoka Wizara ya Afya Zanzibar, Halima Abdulrahman Omar, alisema bado kwenye jamii kuna matatizo mbalimbali ambayo yakiendelea kufichwa hayataondoka.

Alisema matatizo hayo ambayo kwa kiasi kikubwa yanasababishwa na jamii yamekua na athari kubwa kwa wanawake wengi hususani vijijini kukosa haki zao za msingi ambazo wangepaswa kuzipata kama wanaume.

"Kuwapo kwa mazingira hayo kunatokana na malenzi kwa baadhi ya familia ambayo huamini kuwa watoto wa kiume ndio hupaswa kufanya shughuli zote zinazotumia nguvu na kusoma zaidi huku wanawake wakibaki kufanya kazi za nyumbani," alisema.

Aidha, aliwataka wanawake kubadili mtazamo na kuacha kufikiri zaidi kwenye kuwekeza mapambo ikiwamo vitu vya dhahabu na nguo badala yake wanapaswa pia kufikiri kwenye suala la umiliki wa ardhi na nyumba pia kujikita kwenye kilimo.

Baadhi ya washiriki wa mafunzo hayo walisema elimu waliopata kupitia mradi wa viungo imekuja wakati sahihi ukizingatia kuwa watahakikisha wanatoa fursa kwa wake zao na wanawake wengine kwenye jamii kufanya shughuli za kilimo pasi na kuwawekea vikwazo.

## Waziri Mkuya amvaa mwekezaji machimbo

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais Zanzibar, Saada Mkuya Salum, amemtaka msimamizi mkuu wa eneo linalochimbwa kifusi na mawe, Hanyegwa Mchana, Mkoa wa Kusini Unguja, kufuata sheria ili kuepuka athari za kimazingira.

Mkuya alitoa agizo hilo na kumtaka msimamizi huyo, Vuai Ameir Vuai, kutekeleza makubaliano yake na mkataba aliingia kuendesha shughuli hizo, wakati alipotembelea eneo hilo na kutoridhishwa na uendeshaji wa shughuli hizo, hivyo kusababisha malalamiko kutoka kwa wananchi wanaoishi jirani na machimbo hayo.

Alisema umefika wakati kwa serikali kufanya marekebisho ya sheria za maliasili zisizorejesheka ili kunusuru uharibifu wa mazingira lakini pia madhara kwa wananchi.

Mkuya alisema mazingira katika eneo linalochimbwa kifusi hayaridhishi, hasa ukizingatia uwapo wa makazi ya wananchi karibu na machimbo hayo.

Aliitaka Idara ya Mazingira kukaa pamoja ili kufanya marekebisho ya sheria haraka ili kunusuru hali ya mazingira na kufahamisha kuwa hali hiyo imekuwa kutokana na mmiliki huyo kutofuata maagizo aliyopewa na kuwapo kwa udhaifu kwenye usimamizi.

"Hapa inaonyesha kuwa hakuna umakini wala usimamizi madhubuti ndiyo maana mmiliki huyu anafanya kazi zake kwa lengo la kujiimarisha badala ya kujali sheria na athari anazowasababishia wananchi wenzake," alisema.

Pia alisema mwekezaji wa eneo hilo alipaswa kuweka mazingira rafiki kwa wasaidizi wake na wakazi ikiwamo kuweka miundombinu ya uhakika kama njia ili kupitika vyema badala ya iliyopo sasa ambayo inatoa vumbi na kuathiri vyombo vya usafiri, nyumba na hali za wananchi.

Akizungumza wakati wa ziara hiyo, mwekezaji huyo, mbali na kukiri kutochukua hatua za tahadhari, aliahidi kumwagilia maji kila siku ili kupunguza vumbi la njiani linalowaathiri wakazi wa eneo hilo.

Pia alisema pamoja na mamlaka zinazohusika ili kuona namna bora ya kuimarisha miundombinu ya barabara kwa vile kuijenga kwa kiwango cha lami ni gharama kubwa.

Nipashe
MWANGA WA JAMII
BT
BURUDANI TELE
JUMAMOSI MACHI 27, 2021



**TOKE AWALAUMU WANAUME KWA KUCHEPUKA** Ukurasa.14



## YAMETIMIA

# Wasanii watamkumbuka Dk. John Magufuli

HATIMAYE Rais Dk. John Pombe Magufuli, amezikwa kijijini kwake Chato, mkoani Geita jana alasiri.

Watanzania wengi wamefuatilia tukio hilo kupitia runinga wakiwa majumbani kwao, na baadhi walishiriki moja kwa moja katika eneo la tukio.

Walioguswa sana na kifo cha kiongozi huyu shupavu ni wasanii ambao katika uongozi wake walipewa mwongozo thabiti wa namna vipaji vyao vinavyoweza kuwanufaisha kiuchumi.


Baadhi ya wasanii wa muziki na filamu, wametembea mwendo mrefu kutoka mikoa mbalimbali hadi kijijini Chato kwa nia moja tu, nayo ni kumzika jemedari wao.

Wengi wa wasanii wanakiri katika uongozi wa Dk. Magufuli, mambo mengi yamefanyika ikiwamo kukuza sanaa ya muziki na kufufua filamu za Bongo Muvi ambazo zilipoteza mwelekeo.

Chini ya Magufuli, aliweka mkakati wa kuhakikisha vyombo vinavyosimamia sanaa ikiwamo Baraza la Sanaa Tanzania (BASATA) na Bodi ya filamu zinapewa nguvu kiutendaji ili viwanufaishe kiuchumi.

BASI SAWA

## Babu Seya hapati usingizi kwa Magufuli



MWANAMUZIKI mkongwe wa muziki wa dansi, Nguza Viking 'Babu Seya' amesema hajapata usingizi tangu aliposikia kifo cha Rais Dk John Pombe Magufuli.

Kiongozi huyo alifariki dunia Machi 17, mwaka huu kwa matatizo ya moyo.

Babu Seya amesema anafikiria mema aliyomtendea ikiwamo kumtoa jela ambako amefananisha alikuwa kwenye shimo zito lililokuwa limemfunika yeye na familia yake.

## Majizzo yeye si kitu bila utu

MMILIKI kituo cha redio cha Efm, DJ Majizzo, amewakumbusha Watanzania kuwa utajiri na umiliki wa mali si kitu kama mtu hana utu.

Kupitia ukurasa wake wa Instagram, Majizzo, amesema kuna baadhi ya watu ambao wamepata kiwango fulani cha mafanikio wanawadharau wenzao wa chini na kuwaona si lolote.

"Kuwa mkurugenzi na lolote lile ambalo unaniona nalo, haviwezi kuwa na thamani kuliko utu. Labda kuna kiwango cha mafanikio watu wakifika wanadharau wengine, mimi sijakifikia na hata nikifika nitaendelea kuwa huyu kijana wa mtaa anayeendelea kuheshimu vijana wote wa mtaa," amesema wakati alipokwenda kumsalimia kijana anayetembea mikoa yote kuhimiza uzalendo.






## Harmonize ateseka akimkumbuka Magufuli

MSANII wa Bongo Fleva na mmiliki wa lebo ya Konde Gang, Rajabu Abdul Kahali, maarufu kama Harmonize, amesema ni jambo gumu kukubali kuwa Rais John Magufuli ameaga dunia.

Akizungumza baada ya kuaga mwili wa kiongozi huyo akiwa na mpenzi wake Kajala Masanja, Harmonize amesema Magufuli kwake alikuwa kama baba na mwongozaji wake katika mafanikio ya muziki.

Msanii huyo ni mara yake ya pili kuaga mwili wa Dk. Magufuli, katika Uwanja wa CCM Kirumba Mwanza, baada ya kufanya hivyo kwenye uwanja wa Uhuru Dar es Salaam.






## Tanasha afuta kila kitu akimlilia

MAMA mtoto wa Diamond Platnumz, anayefahamika kwa jina la Tanasha, amemuenzi Rais Dk. John Magufuli, kwa kuahirisha tukio ambalo alitaka kulifanya mwezi huu.

Katika ujumbe wake kupitia mtandao wa Instagram, amesema kutokana na msiba huo wa kiongozi imara wa Afrika, hataweza kufanya 'sapraizi' na badala yake anaomboleza akiwa nchini kwao Kenya.

"Nawaahidi 'sapraizi' yangu ambayo nilitaka kufanya jumatano nimeahirisha kutokana na msiba wa kiongozi mkubwa Afrika, nitawapa siku nyingine," ameandika Tanasha.

## Nyimbo 5 zilizoliza watu msiba wa JPM



**Na Adam Fungamwango**

NI tukio la kihistoria ambalo litabaki kuwa kumbukumbu ya vizazi vya sasa na vijavyo kwenye ardhi ya Tanzania. Ni kuondokewa na Rais akiwa madarakani.

Dk. John Magufuli alifariki dunia Machi 17 kwenye Hospitali ya Mzena, Dar es salaam na kuleta vilio na simanzi kubwa kwa Watanzania. Maombolezo yamefanyika kwa njia mbalimbali, ikiwamo nyimbo mbalimbali za muziki wa dansi, bongo fleva na hata kwaya.

Wanamuziki mbalimbali nao waliingia studio kurekodi nyimbo zao ambazo waliona zitafaa kusikilizwa na Watanzania, siku zote za maombolezo. Hizi ni baadhi ya nyimbo ambazo zimeonekana kugusa watu wengi na zimekuwa zikipigwa sana kwenye redio, televisheni na hata kwenye baadhi ya maeneo ambapo msiba uliokuwapo.

**Nenda Magufuli-TOT Plus band**

Ndiyo wimbo bora kabisa wa msiba wa Dk. Magufuli kwa mujibu wa watu wengi waliokuwa wakifuatilia matangazo, waliokuwa wakisikiliza na hata waliokuwa kwenye hafla ya msiba wenyewe.

Ni wimbo iliopigwa na Tanzania One Theatre (TOT), kundi linalomilikiwa na Chama Cha Mapinduzi (CCM).

'Nenda Magufuli' ulioimbwa kwa 'melody' ya simanzi, ukiusikiliza unaweza kukutoa machozi kwa jinsi unavyoimbwa na maneno yake.

Ndiyo wimbo uliowatoa wengi machozi hata pale mjini Dodoma, ambapo kundi hilo lilikuwa likipiga 'laivu' kwenye hafla rasmi ya kitaifa ya mazishi hayo.

Umeimbwa kwenye mirindimo ya Kingoni kwa staili ya kwaya na kama ukiusikiliza sana unaweza ukadhani aliyekuwa kiongozi wa kundi hilo,  Hayati Kapteni John Komba ameimba wimbo huo. Kila mtu anajua kuwa Komba alifariki dunia 2015, lakini waliokuwapo wametenda haki kwenye wimbo huo.

**Tutaonana Magufuli-Peter Msechu**

Ni moja kati ya wimbo unaopendwa kusikilizwa na watu kwenye kipindi hiki cha maombolezo ya mpendwa wetu, Dk. Magufuli.

Msechu amechukua wimbo wasanii wa Nigeria, Prospa Ochimana na Osinachi ambao ni maarufu sana nchini uliotwao 'Ukwueme'.

Alichofanya ni kuubadilisha maneno, yakawa na kiswahili na kuimba kutokana na mukhtadha uliokuwapo na msiba huo. Kifupi tu unaweza kusema ni kama 'remix' yake.

Nao pia umegeuka kuwa moja ya wimbo bora wakati huu wa maombolezo.

**'Kalale Pema Magululi'-Tanzania All Stars**

Huu ni muziki wa dansi. Wanamuziki wa dansi waliungana siku moja tu baada ya kifo kutangazwa, na kutoa wimbo uitwao 'Kalale Pema Magufuli.'

Baadhi ya wanamuziki walioingia studio kutoa kibao hicho ni mwanamuziki mkongwe nchini aliyekuwa akiipigia DDC Mlimani Park, Maximillian Bushoke, Abdallah Hemba, Mackey Fanta, Samat Rajabu, Ramadhani Mhoja, Matei Joseph, Jado FFU, Abdallah Tungwa, Liva Sultan, Jimy Manzaka, Mule FBI, Trsia Masela, Mwezi Mpya, Achuda Bikoo, Shomari Ally, Mjusi Shemboza, Kassim Mafanya, Yusuph Subwa na Kanku Kelly.

**'Ahsante Magufuli'-Konde Music Artist**

Harmonize akiwa na kundi lake la Konde Music Artist wametoa wimbo pia wa kumlilia Magufuli, msanii Mbosso akiwa mmoja wa waliotia sauti kwenye wimbo huo, pamoja na wasanii wengine wa kundi hilo.

**'Bye Bye Magufuli'-Aslay**

Msanii Aslay naye hakuwa nyuma. Akatoa pia wimbo wake wa kumlilia Dk. Magufuli na kuwa mmoja wa wanamuziki ambao walitoa mchango wa nyimbo kwenye msiba huo mkubwa wa kitaifa.

## Hulka; Mwana kulitafuta, mwana kulipata

**Na Adam Fungamwango**

MTU anaweza kujifanya mjuaji na kufanya mambo mengi ya kujifurahisha nafsi, lakini ni mambo mabaya na najsi mbele ya Mwenyezi Mungu, lakini kumbe huwezi kujua mbele ya safari hatam yake itakuwa nini.

'Hulka' ni filamu ambayo inamhusu dada mmoja aliyelazimisha kuolewa na mwanamume, lakini lengo haikuwa ndoa. Alikuwa na kitu tofauti moyoni mwake.

Kwa sababu wenzake wote wameolewa? Kuondoa mkosi? Au awe na kwa kujishikiza?

Waliocheza filamu hii ni Madebe Lidai, Mohamed Nurdin maarufu kama Chekibudi, Suleiman Barafu, Anwar Nassor na wengineo.

Inaanza kuonyesha kuwa Anwar anakwenda nyumbani kwa rafiki yake Madebe. Hamkuti, lakini anamkuta mkewe. Anamuuliza shemeji yake kama ana mwanamke au la jambo ambalo linamshangaza Anwar.

Anamjibu shemeji yake kuwa alikuwa na mwanamke, lakini kwa sasa wameachana.

Hidaya ambaye ni mke wa Medebe anamwambia shemeji yake Anwar kuwa kesho wakutane kwenye njia ya kwenda kisimani kuna kitu anataka kumwambia, wanakubalia.

Wanakutana kesho yake, Hidaya anamwambia shemeji yake kuwa anampenda. Anwar anashangaa na kumuuliza shemeji yake kwa nini anataka kumsaliti mumewe?

Anamjibu kuwa yeye hahofii hilo, ila kwa sasa anachotaka wakubaliane wawe wapenzi. Inakuwa hivyo. Hata hivyo wakati wanazungumza kuna mtu ambaye kidogo ana matatizo ya akili 'chizi wa mtaa' alikuwa akiwasikia.

Baada ya miezi sita Hidaya anapata ujauzito. Mumewe Madebe anafurahi sana na kuahidi kumtafutia zawadi kubwa mkewe kama atajifungua salama.

Siku moja Madebe anaangusha pochi, inayookotwa na chizi. Bila kuangalia ndani kuna nini anamrudishia Madebe nyumbani kwake. Anamshukuru, lakini chizi huyo anaondoka akiwa anaongea maneno ya mafumbo ambayo Madebe hajui maana yake.

Hidaya anaomba ruhusa kwenda kijijini kwao kumuona shangazi yake mgonjwa.

Anaporuhusiwa, badala ya kwenda huko alikoomba anaenda kwa hawara yake Anwar, akipika na kupakua bila kujali watu wanaomuona.

Baada ya wiki moja kupita, Madebe anapokea taarifa za msiba kutoka ukweni kuwa shangazi amefariki, hivyo anatakiwa kumtaarifu pia na mkewe waende mazishini.

Madebe hashangazwi na taarifa za kifo, ila kuambiwa amtaarifu mkewe ambaye tayari anajua yupo huko.

Mwisho wa siku anaamua kwanza kwenda kwa rafiki yake Anwar ili akamuelezee jambo hili kabla hajaondoka.

Alipofika, alishangazwa kuona nguo za mkewe zikiwa zimeanikwa nje, lakini alipogonga hodi mkewe alitoka pamoja na rafiki yake Anwar.

Hata hivyo, chochote walichotegemea sicho. Madebe aliwasamehe na kumchukua mkewe akarudi naye nyumbani.





# The Game ataka wanaotaka kuoa mke wafunge mitandao

RAPA wa Marekani, Jayceon Terrell Taylor, ambaye anafahamika kama 'The Game', ametoa ushauri kama mwanaume anataka kumpata mke bora, kwanza afute ukurasa wake wa Instagram.

Nyota huyo wa muziki ametoa ushauri huo kupitia akaunti yake ya Twitter, kwamba kuna wanawake wengi wazuri wanaozaliwa kila kukicha na endapo unatafuta mwenza inabidi kutumia akili na sio mitandao ya kijamii.

"Kuna wanawake wengi wazuri duniani, hasa katika kipindi hiki kila ukimuona unaona Yule wa kwanza ni mbaya, nafikiri endapo unatafuta mke ni lazima kufuta Instagram yako," amesema.



## Toke alaumu wanaume kwa kuchepuka

MWIGIZAJI wa filamu, Toke Makinwa, amesema mwanamke hapaswi kulaumiwa katika makosa ya wenza kutoka nje ya ndoa.

Katika mjadala unaoendelea katika mitandao ya kijamii kuhusu nani wa kulaumiwa pale mwanaume anapotoka nje ya ndoa.

Msanii huyo wa filamu na pia mwanamitindo, amesema wanaume wanajidhalilisha kwa kudanganya wenzi wao wakati akiwa na mchepuko ndani ya ndoa.

## Koffi Olomide amlilia Magufuli

MWANAMUZIKI mkongwe kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Koffi Olomide, ameungana na Watanzania kuombeleza kifo cha Rais Dk. John Magufuli.

Kupitia video fupi aliyoiweka katika ukurasa wake wa Istagram, Olomide, amesema amehuzunishwa na msiba huo mzito na yupo pamoja na Watanzania katika kipindi hiki kigumu.

Koffi amekuwa akija kila mara Tanzania kwa ajili ya kufanya maonyesho mbalimbali ya kimuziki pamoja na kushiriki katika nyimbo za wasanii Diamond Platnumz na Nandy.





## Kevin Hart kweli mtoto kwa baba hakui

MSANII wa uchekeshaji wa Marekani, Kevin Hart, ameonyesha nguvu ya fedha baada ya kumzawadia binti yake gari la kifahari aina ya Mercedes Benz SUV, akitimiza miaka 16 ya kuzaliwa kwake.

Staa huyo wa filamu alifanya jambo hilo kama sapraizi kwani hakuna mtu katika familia yake aliyefahamu kuhusu zawadi hiyo.

Heaven ambaye ni binti wa kwanza wa msanii huyo amepewa gari hilo lenye thamani ya dola za Marekani 47,000 sawa na sh. milioni 109.


## Prince Harry kuanza kazi mpya

MWANAMFALME Harry ameelezwa amepata kazi mpya ya ukurugenzi katika kampuni ya Silicon Valley.

Katika chapisho lake katika jarida la Wall Street Journal, Prince Harry, atachukua nafasi hiyo kama ofisa mkuu wa BetterUp Inc, akisaidia mafunzo ya afya ya akili.


"Nina nia ya kusaidia kuondoa athari katika maisha ya watu. Kufundisha kwa bidii kunatoa uwezekano mkubwa wa maendeleo ya kibinafsi, kuongezeka kwa mwamko, na maisha bora kote, "alisema.






# BURIANI JPM KIPENZI CHA WASANII

**Na Habbi Gunze**



HAIKUWA rahisi kuamini kuwa Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania, Dk. John Magufuli, kuwa amefariki dunia. Nilipata mshituko mkubwa na majonzi yasiyoelezeka Machi 17, 2001 usiku wakati Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan alipoonekana kwenye televisheni akitangaza kuwa JPM hatunaye tena, ametangulia mbele za haki kwa maradhi ya moyo.

Usiku ule sikupata usingizi hadi asubuhi. Niliwaza na kuwazua. Kesho yake nilianza kufikiria mstakabali wa taifa bila JPM. Nikajikusanya akili yangu ikakaa sawa. Nikatoa agizo ofisini kwa Katibu Mtendaji kuwa Baraza la Sanaa Tanzania (BASATA) atoe taarifa ya salamu za rambirambi kwa Samia na kwa Mama Janet Magufuli na familia. Na kweli BASATA walifanya hivyo.

Lakini bado kichwani mwangu kulikuwa na mambo mengi juu ya sanaa ya Tanzania bila JPM. Niliwaza sana kwa sababu ya matumaini ambayo JPM alikuwa ameanza kuweka ndani ya sanaa na wasanii kwa vitendo vyake vya upendo na kuthamini kazi za sanaa. Kwa nyakati tofauti za utawala wake, aliweka hadharani ahadi za kuinua tasnia ya sanaa ili ifikie kiwango cha juu na kushindana kimataifa.

Alipoingia madarakani Novemba 5, 2015 baada ya kuapishwa, alipowasili Ikulu kabla ya kuingia ndani, alipiga ngoma mlangoni kuashiria kuwa mtawala wa nchi kaingia Ikulu.

Ngoma hizo alizipiga kwa ufundi na bashasha tele kuonyesha kuwa alikuwa anafurahia sana kitendo hicho. Hii ilikuwa ishara nzuri kwa tasnia ya sanaa kuwa ndani ya Ikulu sanaa imepata mtetezi. Ndivyo ilivyojidhihirisha miaka iliyofuata ya utawala wake kuwa alikuwa mpenzi wa sanaa.

JPM alikuwa na maono makubwa juu ya maendeleo ya sanaa nchini. Novemba 15, 2019 wasanii walipokuwa katika Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Julius Nyerere (JNICC), Dar es Salaam kwenye Tamasha la Sanaa la Mwalimu Nyerere, kupitia kwa Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, ambaye alikuwa mgeni rasmi, Dk. Magufuli, ambaye alikuwa anaangalia tamasha mubashara Ikulu, aliushangaza umati alipopiga simu kwa Majaliwa na kusema amefurahishwa sana na tamasha hilo na michango inayotolewa na wadau kuanzisha Mfuko wa Utamaduni na Sanaa.

JPM alitamka hapo hapo kuwa anachangia Sh. milioni 100 kutunisha mfuko huo. Katika tamasha hilo Sh. 147,050,000 zilichangwa kutunisha mfuko huo. Mchango huo wa JPM si tu kwamba alionyesha upendo mkubwa kwa wasanii bali pia alionyesha thamani ya sanaa na wasanii wenyewe.

JPM alijua kuwa tasnia ya sanaa na burudani ina uwezekano mkubwa wa kuingizia nchi mapato mengi na kutengeneza maelfu ya ajira siku za mbele ikiwa serikali itaipa kipaumbele katika kuwekeza kwenye miundombinu na mifumo ya maendeleo ya sanaa.

Katika ripoti ya serikali ya hali ya uchumi ya mwaka 2019/2020 sekta ya sanaa na burudani ilikuwa kwa asilimia 13.7, hivyo kuongeza mchango wake katika pato la taifa kuliko ilivyokuwa miaka ya nyuma.

Serikali kuanzia miaka ya hivi karibuni, imeanza kuweka vipaumbele katika kuboresha mambo kadhaa yanayohusu maendeleo ya sanaa ikiwa ni pamoja na upatikanaji wa mazingira bora ya wasanii kufanya kazi zao, mfumo bora zaidi wa usajili wa wasanii, uwepo wa miundombinu ya kufanyia kazi za sanaa, mfumo bora zaidi wa kupata maslahi ya wasanii kulingana na kazi zao, ulinzi wa kazi za sanaa na uanzishwaji wa mfumo wa kielektroniki wa kukusanya mapato ya kazi za sanaa.

Baadhi ya hatua za JPM kuimarisha sanaa nchini ni pamoja na agizo lake la kuweka Chama cha Hakimiliki Tanzania (COSOTA) chini ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo na kuitoa chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara.

Sasa taasisi zote zinazohusika na kuhudumia sanaa na wasanii yaani, BASATA, Bodi ya Filamu na COSOTA ziko chini ya wizara moja. Hii italeta ufanisi wa kazi na tija kwa wasanii na wadau wengine.

Bado kuna haja, katika mazingira ya sasa, serikali na wadau wa sanaa kufikiria kama ni vyema kuendelea kuwa na taasisi tatu za kushughulikia sanaa badala ya kuwa na taasisi moja yenye nguvu na uwezo mkubwa wa kushughulikia mambo yote ya sanaa kwa ufanisi na tija kubwa zaidi.

Mfumo na utaratibu wa kuunganisha vyombo kadhaa vinavyohudumia sekta moja ni muhimu kwa uchumi wa taifa na wale wanaohudumiwa kwa sababu wanapata huduma katika sehemu moja.

Serikali inapunguza matumizi, ufanisi wa huduma unakuwa wa uhakika kwa vile huduma zinakuwa ni sehemu moja. Tija inakuwa ya uhakika kwa sababu ya kuwa na chombo kimoja na hivyo matumizi yanapungua na mapato yanaongezeka.

Katika upande wa weledi, chombo kimoja kinakusanya utaaalamu sehemu moja na hivyo weledi wa utoaji huduma unaboreka.

Katika kampeni za uchaguzi mwaka 2020, Chama Cha Mapinduzi (CCM) kupitia aliyepeperusha bendera ya CCM, Dk. Magufuli, kiliwathamini sana wasanii na kuwa nao pamoja katika ziara zote za kampeni hizo.

Hii ilikuwa na maana ya kuwa wasanii ni sehemu ya utamaduni na siasa ya nchi hii. Lakini pili, wasanii wana ushawishi mkubwa sana katika kuhamasisha wananchi kwa kupitia nyimbo. CCM ililitambua hilo na ndiyo maana wasanii walikuwa hawakosi kwenye mikutano ya kampeni ya JPM.

**IMANI KWA SAMIA**

Wadau wa sanaa wana imani kubwa sana na Rais Samia Suluhu Hassan, kwanza, kwa kuwa alikuwa mgombea mwenza wa JPM na sasa yeye ni Rais amekuwa ndiye kinara wa kutekeleza yale yaliyomo kwenye Ilani ya Uchaguzi ya CCM. Hakuna shaka yoyote kuwa sanaa na wasanii wataendelee kufanya kazi zao kwa kujiamini kwa vile Samia ataendeleza upendo aliokuwa nao JPM kwa wasanii na sanaa kwa jumla kwa sababu ndiyo sera ya CCM.

Wadau wa sanaa na wasanii wako tayari kushirikiana na Rais Samia ili kuimarisha tasnia ya sanaa na kuiweka katika kiwango cha juu.

Wasanii na wadau wa sanaa watakumbuka sana upendo wa JPM hasa alivyokuwa anajumuika nao kwenye majukwaa kutoa burudani kwenye hafla mbalimbali. Hii ilikuwa haiba ya pekee aliyokuwa JPM kwenye Sanaa. Hii ni kwa sababu ya mapenzi makubwa aliyokuwa kwenye sanaa na utamaduni wa Mwafrika.

Hivi karibuni, Februari 25 wakati anazindua kituo cha televisheni cha Channel TEN, akikagua studio, ghafla aliomba apigiwe wimbo wa Profesa Jay na Stamina wa "Baba".

Kila mtu kwenye msafara wake alishangaa, Rais pamoja na kazi na shughuli nyingi za majukumu ya urais, anapata muda wa kusikiliza nyimbo za wasanii wa Kitanzania na hasa za Bongoflava.

Kwa kweli JPM alikuwa kipenzi cha wasanii wa Kitanzania. Kwa kujua kuwa JPM alikuwa anawathamini wasanii wa Kitanzania, mara zote BASATA haikuwa inawaomba au inawashinikiza kutunga nyimbo za kusifia na kuthamini michango ya JPM katika kutekeleza miradi ya maendeleo ambayo imeiweka Tanzania katika uchumi wa kati. Wasanii wenyewe waliona kazi nzuri inayofanywa na JPM.

**Pumzika Shujaa wa Afrika, Lala salama kipenzi cha Wasanii.**

hgunze@gmail.com
+255 655 337 337

# Madeni aliyoacha JMP yanamhusu Rais Samia

**Beatrice Moses**

AHADI ni deni ni mojawapo ya misemo wa wahenga ambao pia hukolezwa kwa mwingine usemao "dawa ya deni ni kulipa".

Tumeshuhudia vilio, taharuki, huzuni na maombolezo ya aina yake wananchi wengi wakimlilia Hayati Dk John Magufuli aliyefariki dunia Machi 17, mwaka huu na anazikwa Machi 26 kijijini Chato mkoani Geita.

Ni kama utamaduni fulani hivi kweye misiba kadhaa ambayo nimewahi kuhudhuria nilisikia kiongozi wa familia mara baada ya shukrani au kabla ya shukrani kwa waombolezaji hutangaza kama kuna mtu alikuwa anamdai au anadaiwa na marehemu hajitokeze ili taratibu nyingine ziweze kufanywa ikiwamo utaratibu wa kulitambua deni na kulipa.

Ni wazi kwamba msiba wa Dk. Magufuli ni wa kipekee kwa kuwa ndiyo rais wa kwanza nchini kufa akiwa madarakani, hivyo nafasi yake ni tofauti na ya misiba mingine, huu ni msiba mkubwa kwa hakika hivyo huwezi tarajia kuwapo kwa swali la nani alikuwa anamdai au anadaiwa na Hayati JPM.

Huyu ni kiongozi ambaye licha ya kujitoa kwa kiwango cha juu katika kuhakikisha anatimiza ahadi zake, lakini amekufa ghafla hivyo ameacha maswali mengi hasa miongoni mwa wananchi wanyonge ambao tayari walikuwa wamepata tumaini la kupiga hatua ya maendeleo kwenye sekta tofauti.

Machozi ya Watanzania wengi ni wazi yana sababu nyingi haibadilishi ukweli kuwa yanasababishwa na uchungu wa kuondokewa na kiongozi waliyemwamini ambaye anatajwa kuwa shujaa wa Afrika ambapo amethibitisha kuwa alikuwa shujaa kwa vitendo vyake.

Dk Magufuli amekufa ghafla machozi ya wanyonge hata maneno yako wanathibitisha kuwa walikuwa wanamtegemea aendelee kuwalipa aliyowahahidi wakati wa kampeni awamu ya kwanza na awamu ya pili ambayo ameitumikia kwa miezi minne siku kadhaa tu kisha akakutwa na mauti.

Juhudi kubwa alizofanya katika kuhakikisha analipa madeni ya ahadi zake kwa wananchi wake, ambapo kwa awamu ya kwanza wananchi wameshuhudia akitimiza ahadi nyingi kati ya alizoahidi.

Ni wazi wapo waliobeza kuwa alizitoa ili achaguliwe tu, lakini yeye alizitimiza kudhihirisha dhamira yake njema ya kuwatumikia wananchi.

Miongoni mwa ahadi alizotoa ni pamoja na elimu bure, ujenzi wa miundombinu, kuwa na usafiri wa anga na viwanja vya kisasa, kutetea haki za wanyonge, kuifanya Tanzania kuwa nchi ya viwanda na kuinua uchumi wa nchi, kuimarisha huduma za afya na kuhakikisha wananchi wanapata nishati na maji safi na salama.

Ahadi hizo na nyinginezo ndiyo ziliwashawishi na kusababisha wananchi kumwamini na kumchagua kwa kura nyingi katika uchaguzi mkuu uliofanyika Oktoba mwaka 2020 ambapo alitagazwa na Tume ya Uchaguzi kuwa alishinda kwa asilimia 84.



Baada ya kusikia taarifa za kifo chake wananchi wengi walichanganyikiwa, huzuni na vilio vilitawala kila kona ya nchi, tumeshuhudia kupitia vyombo vya habari hadi baadhi ya wanaume wakiangua kilio hasa baada ya kushuhudia mwili wa JPM ukiwa ndani ya jeneza.

Wananchi kadhaa waliohojiwa na vyombo vya habari tofauti wakati wa shughuli ya kuaga mwili wake, wengi walieleza jinsi gani kifo cha Dk. Magufuli kimewaumiza pia ni namna gani watamkumbuka.

Hayati Rais Dk. Magufuli wakati akifungua rasmi Bunge la Kumi na Moja Novemba 20 mwaka 2015 aliahidi kutekeleza ahadi alizotoa, wakati wa kampeni za uchaguzi, licha ya kuwapongeza wabunge kwa kuchaguliwa pia aliwakumbusha kuwa wananchi wanasubiri kuona madai yao yamesikilizwa na kutekelezwa na hivyo wanahitaji uwajibikaji wa watu wote.

"Sisi sote watatupima kwa namna tutakavyokidhi kiu na matarajiyo yao. Na sote tuliahidi kuwatumikia wananchi. Na kutokana na utumishi wetu kwao tuweza kutatua matatizo mbali mbali."

Alisema wananchi wamechoshwa na vitendo vya rushwa, alipowaahidi kushughulikia suala hilo hakuahidi ili kuwarubuni wampe kura bali ndicho alichomaanisha.

Dk. Magufuli alisema vitendo vya rushwa na ufisadi vimewanyima haki wananchi na kuitia hasara serikali

" Wananchi hawapo tayari kuvumilia upuuzi wa Serikali inayolea rushwa na kulea mafisadi , nataka nirejee ahadi yangu,

nimewaahidi wananchi kuwa nitapambana na rushwa, dawa ya jipu ni kulitumbua, nami nimejipa kazi ya kutumbua jipu,"alisema.

"Nafahamu ugumu wa vita niliyoamua kuipigana kwa sababu wanaojihusisha na rushwa siyo wadogowadogo, hutendwa na watu wenye dhamana za uongozi na utumizi ambazo wamezipata kutokana na ridhaa ya watu.

Alisema katika kushughulikia tatizo hili aliahidi kuunda Mahakama ya Rushwa na Ufisadi aliamini vyombo husika havitanikwamisha katika kufanikisha hilo.

"Kiongozi yeyote wa kuteuliwa ambaye mimi nitakuwa nimemteua kwa mamlaka niliyonayo kikatiba na ninayo mamlaka ya kumwajibisha, pindi nikibaini anajihusisha na rushwa na ufisadi nitamtimua mara moja wala sitakuwa na kigugumizi," alisema.

Hayati Magufuli alichokisema alimaanisha kwani enzi za uongozi wake wananchi wameshuhudia viongozi kadhaa mwenye nyadhifa tofauti wakiwamo mawaziri wakiondolewa kwenye nafasi hizo baada ya kubainika kushindwa kusimamia kazi zake hivyo kusababisha mambo kukwama ama kuharibika.

Hivi karibuni kumeibuka kashfa dhidi ya baadhi ya polisi wa Kituo cha Polisi Buguruni wilayani Ilala, ambapo baadhi ya wafanyabiashara wa nyama waliokamatwa kwenye msako uliohusisha Bodi ya Nyama wakisaka ambazo hazikugongwa muhuri wa kuthibitisha zinafaa kuliwa. Wafanyabiashara hao wamelalamikia kuwa nyama zilizokamatwa hawakurejeshewa licha ya kuwa walilipishwa faini wakapewa na risiti, lakini wakadai nyama hizo zinazokadiliwa kufika kilo 800 polisi waligawana kisha wakadai kuwa zimeteketezwa.

Mgendi Matutu ni mmoja wa wafanyabiashara waliodai kunyang'anywa nyama za biashara huku akieleza siku Rais Magufuli akifika, pengine ndipo wangepata haki yao hiyo waliyodai imepokwa na polisi hao.

Kauli hiyo aliitoa akiamini kuwa kutokana na msimamo wa Hayati Magufuli ni wazi polisi wote waliohusika wangebanwa na hatua zaidi zingechukuliwa ili kukomesha vitendo vya namna hiyo.

Hii ni mojawapo tu ya mambo ambayo husababisha majeraha kwenye mioyo ya wananchi, Sasa Rais ni Samia ambaye ndiye alikuwa Makamu wa Rais anatambua wajibu wake kwa kuwa ni Mwanamke jasiri mwenye uwezo mzuri wa kujieleza na kutenda na kufuatilia.

Wakati wa kampeni mwaka 2015 nilikuwa ni miongoni mwa waandishi walioripoti habari kutoka kwenye safari za kampeni zake hivyo nilishuhudia jinsi naye alivyokuwa akitoa ahadi za kuwashawishi wananchi kumchangua Dk. Magufuli ili aweze kushirikiana naye katika kuzitekeleza kwa maendeleo ya taifa.

Sasa yeye ndiyo Rais hivyo pamoja na mambo mengie naamini ana uwezo wa kuhakikisha Jeshi la Polisi alichafuliwi na wachache wenye uchu na wanaojali maslahi yao kiasi ya kupora vidhibiti na kugawana ni wazi kuwa kuna utaratibu wa kuteketeza vidhibiti ambavyo vilipaswa kufuatwa siku hiyo.

Rais Samia anatambua wananchi wana kiu ya kuona yale aliyoyaanzisha Hayati Magufuli ambapo walikuwa wakiyatekeleza kwa wake hasa kwa pamoja katika nafasi yake ya makamu wa Rais, hivyo ahadi hizo walizotoa kwa pamoja katika maeneo tofauti nchini wakati wakiomba ridhaa kwa wananchi.

Rais Samia akihutubia kwenye mazishi ya kitaifa yaliyofanyika jijini Dodoma alisema "siku nyingine ngumu katika historia ya nchi yetu, ila kwangu ni ngumu zaidi, ilianza ugumu tangu nilipotangaza kifo cha Rais, nilihisi nafanya makosa kumtangaza Rais wangu, Siwezi kusahau mchango wa Rais Magufuli katika maisha yangu ya kisiasa."

Alimshukuru Hayati Dk Magufuli kwa kumwamini na kwa wanawake wa Tanzania, aliiandika historia ya usawa wa kijinsia kwenye nyanja za siasa nchini.

Alibainisha kuwa Rais Magufuli hakuogopa kutetea kile alichoamini kuwa ni sahihi kwa maslahi ya Taifa hata kama kingehatarisha maisha. "Naomba niseme kidogo, kwa wale wenye mashaka na mimi kwamba mwanamke huyu atweza kuwa Rais wa Tanzania, nataka niwaambie kuwa aliyesimama hapa ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye maumbile yake ni mwanamke," alisema Rais Samia akifuatiwa na sauti za kushangiliwa kwa makofi na vigelegele.

Aliwaeleza waombolezaji kuwa wamepoteza kiongozi mahiri, shupavu, jasiri, mchapakazi, mwadilifu, mnyenyekevu, mcha Mungu, mfuatiliaji, mzalendo kwa Taifa lake, mtetezi wa wanyonge, mwana mwema wa Afrika, mwana mapinduzi, mwana mageuzi na mtumishi wa wote.

"Tunapoenda kumpumzisha, sisi viongozi tunaahidi kwamba tutaendeleza kazi yake nzuri kwa nguvu na kasi ile ile, Kwa tuliomfahamu na kupata fursa ya kuishi nae tuliona unyenyekevu, upendo na huruma yake uvunguni mwa taswira yake ya ukali tuliyoiona katika matamshi yake,"

Katika hotuba yake hiyo Rais Samia alisema Hayati Dk Magufuli

alikuwa sio tu kiongozi tu, bali pia mzazi na mlezi kwa wengi, mwenye kusamehe, kuvumilia, kulea sana na mkweli.

"Aliamini kwenye kuhakikisha Watanzania wote wanapata haki ya usawa wa kujitafutia riziki ya halali popote nchini, hivyo alirasimisha sekta isiyo rasmi na kuweka sekta wezeshi kwa wafanyabiashara na wajasiriamali wadogo kufanya kazi zao,"Alisema Rais Samia.

HABARI KIMATAIFA

# Korea Kaskazini yajigamba kumiliki kombora la kisasa

**PYONGYANG, Korea Kaskazini**

KOREA Kaskazini imedai kuwa makombora iliyoyafyatua juzi, Alhamisi yaliongozwa kwa kifaa kinachotumia teknolojia mpya.

Katika taarifa yake ya kwanza tangu ilipotekeleza jaribio hilo iliyotolewa kupitia vyombo vya habari vya kitaifa, ilisema silaha hizo mbili zilipiga eneo lililolengwa lililopo umbali wa kilomita 600 sawa na maili 373 kutoka kwenye mwambao wa mashariki mwa nchi hiyo.

Hata hivyo, Japan ilipinga taarifa hiyo ikisema makombora hayo yalipaa zaidi ya kilomita 400 pekee.

Ulikuwa ni uzinduzi wa kwanza wa nchi hiyo wa makombora ya masafa marefu tangu Rais Biden aingie madarakani.

Rais wa Marekani, Joe Biden alisema baada ya tukio hilo kuwa Marekani itajibu ipasavyo.

Tarari Japan na Korea Kusini imeungana na kiongozi huyo kulaani majaribio hayo.

Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa, katika azimio lake imeipiga marufuku Korea Kaskazini kufanya majaribio ya makombora ya masafa marefu.

Katika taarifa hiyo, iliongeza kuwa aina mpya ya makombora hayo yanaweza kubeba mzigo wa tani 2.5 , ikiwamo vichwa vya nyuklia.

Vyombo vya habari vya taifa hilo vilitoa picha za majenerali wa jeshi la Korea Kaskazini wakifurahia jaribio hilo

"Utengenezaji wa mfumo wa silaha hii ni wa muhimu katika kuonesha uwezo wa kijeshi wa nchi na kuzima aina zote za vitisho vya kijeshi ," alisema Ri Pyong Chol, ofisa wa ngazi ya juu ambaye alishuhudia jaribio hilo.

Hata hivyo, kiongozi wa Korea Kaskazini Kim Jong-un hakuwapo wakati wa tukio hilo.

Baada ya tukio hilo, Rais Biden aliwaambia waandishi wa habari kwamba ufyatuaji wa makombora hayo ulikuwa ni ukiukaji wa maazimio ya Umoja wa Mataifa na kwamba Marekani inashauriana na washirika wake kuhusu tukio hilo.

"Kutakuwa na jibu kama wataamua kuendeleza ufyatuaji huo, tutajibu ipasavyo," alisema.

Aliongeza "lakini pia nimejiandaa kwa aina fulani ya diplomasia, lakini lazima iwe na masharti ya kwamba matokeo yake yawe kuzuiwa kwa matumizi ya nyuklia Korea Kaskazini."

Bado haijaeleweka wazi ni aina gani ya makombora ambayo yamefyatuliwa na Korea Kaskazini. Vyombo vya habari vya taifa hilo vimesema kombora hilo lilikuwa la aina iliyoboreshwa ya injini ngumu ya mafuta.

Ilielezwa makombora hayo yaliongozwa kimkakati na kuwa na uwezo wa kukwepa pale inapotaka kutunguliwa.

Jaribio hilo linaonyesha mafanikio katika mpango wa nchi hiyo wa silaha za nyukli tangu mazungumzo ya kusitishwa chini ya utawala wa Marekani wa Donald Trump.

**BBC**



Kombora jipya lenye uwezo wa kubeba zana ya nyuklia likirushwa kwa majaribio na Korea Kaskazini siku ya Alhamisi **PICHA: AFP**

## Ethiopia yasema Eritrea inaondoa wanajeshi Tigray

**ADIS ABABA, Ethiopia**

WAZIRI Mkuu wa Ethiopia, Abiy Ahmed, amesema nchi ya Eritrea imekubali kuondoa wanajeshi wake kutika jimbo la Tigray.

Hatua hiyo imekuja baada ya kuwapo kwa ushahidi kuwa wanajeshi hao wamepora, kuua na kubaka raia wakati wa mapigano ya kukomboa eneo hilo.Taarifa iliyotolewa na ofisi ya kiongozi huyo, ilitolewa baada ya kuwapo shinikizo kutoka kwa Marekani na viongozi wengine duniani kuitaka Ethiopia kushughulikia mgogoro katika jimbo la Tigray.

Makubaliano hayo yalifikiwa baada ya ziara ya waziri mkuu Abiy Ahmed nchini Eritrea, na kutangaza kuanzia sasa wanajeshi wa Ethiopia watalinda maeneo ya mpakani.

Wiki iliyopita, Abiy alikiri uwapo wa vikosi vya usalama vya Eritrea, ambao wanafahamika kuwa wapinzani wa muda mrefu wa viongozi wa Tigray, waliokuwa na ushawishi mkubwa katika serikali ya Ethiopia.Hata hivyo, Eritrea haijasema lolote kuhusu kauli hiyo.

**DW**

## Maandamano yazidi kuitafuna Myanmar

**NAYPYIDAW, Myanmar**

MAMIA ya raia wa Myanmar wameendelea kufanya maandamano jana baada ya jeshi kuripotiwa kuwauwa kwa kuwapiga risasi watu tisa.

Vyombo vya habari nchini humo viliripoti kuwa maandamano yalifanyika katika sehemu mbalimbali ikiwemo mji wa pili kwa ukubwa wa Mandalay.

Maandamano hayo yalitokea katika wakati ambapo benki kuu ya dunia imeonya kuwa uchumi wa nchi hiyo huenda ukadorora kwa asilimia 10 kutokana na mzozo unaoendelea.

Kama njia ya kuongeza shinikizo kwa jeshi kufuatia mapinduzi ya Februari mosi, Marekani na Uingereza ziliwawekea vikwazo baadhi ya viongozi wa jeshi, hatua ambayo ni kama jibu kwa ukandamazaji unaofanywa na jeshi.

Nchi hiyo imekumbwa na maandamano karibia kila siku baada ya jeshi kuipindua serikali ya Aung San Suu Ky iliyochaguliwa kwa njia ya demokrasia.

**DW**

## Hukumu ya kifo yafutwa Virginia

**VIRGINIA, Marekani**

BUNGE la jimbo la Virginia, limefuta hukumu ya kifo baada ya chama cha Demokratic kushinda.

Hukumu ya kifo ilifutwa kutokana na kutimiza ahadi ya wabunge wa chama hicho wakati wa uchaguzi.

Gavana, Ralph Northern, alitia saini muswada wa kupiga marufuku hukumu ya kifo, uliopitishwa na bunge la serikali na kusema hilo ni jambo la maadili limetekelezwa.

Virginia lililokuwa jimbo la 23 nchini humo kuchukuwa uamuzi huo, limekuwa la kwanza kupinga hukumu ya kifo kati ya majimbo ya kusini ambayo yamekuwa yakitekeleza adhabu hiyo mara kwa mara.

Tangu kuanzishwa kwake mwaka 1608, jimbo la Virginia lilishika nafasi ya kwanza kati ya majimbo 50 nchini Marekani kwa kutekeleza takriban hukumu 1,400 za kifo.

**DW**

## HABARI PICHA

# MAOMBOLEZO YA HAYATI JPM KATIKA PICHA



Rais Samia Suhulu Hassan, akiwasili wilayani Chato mkoani Geita jana, kwaajili ya kuhudhuria mazishi ya Hayati Dk. John Magufuli. **PICHA: IKULU**



Mkuu wa Wilaya ya Simanjiro, mkoani Manyara, Mhandisi Zephania Chaula, akizungumza kwenye sala na dua ya kumwombea mapumziko mema aliyekuwa Rais, hayati Dk. John Magufuli, wilayani humo juzi. **PICHA: GIFT THADEY**



Vijana wa halaiki Wilaya ya Muheza, wakiimba wimbo wa Taifa, kabla ya ibada ya kumwombea aliyekuwa Rais, Hayati Dk. John Magufuli katika Uwanja wa Jitegemee, wilayani humo, mkoani Tanga jana. **PICHA: HAMIDA KAMCHALLA**



Mkuu wa Wilaya ya Muheza, mkoani Tanga, Mhandisi Mwanaasha Tumbo, akitia saini kitabu cha maombolezo kabla ya kuhudhuria ibada maalum ya kumwombea hayati Dk. John Magufuli katika Uwanja wa Jitegemee jana. **PICHA: HAMIDA KAMCHALLA**



Mwenyekiti wa wawakilishi wa wanajeshi kutoka nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki, Kanali Rafael Kiptoo, akizungumza na waandishi wa habari, baada ya kutia saini kitabu cha maombolezo ya kifo hayati Dk. John Magufuli, katika ofisi ya Mkuu wa mkoa wa Arusha juzi. **PICHA: WOINDE SHIZZA**



Chifu Adam wa Pili wa Kabila la Wahehe, mkoani Iringa, Adam Abdul Adam Sapi Mkwawa, akitia saini kitabu cha maombolezo ya kifo cha aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Tanzania, hayati Dk. John Magufuli, katika Ofisi ya Mkuu ya Mkoa Iringa mapema wiki hii. **PICHA: FRIDAY SIMBAYA**

## HADITHI

# HADITHI

MAUAJI ya kutisha yanatokea ndani ya gesti moja maeneo ya Kigogo jijini Dar es Salaam. Mfanyabiashara Burhan anauawa ndani ya gesti ya Tukutane, akiwa na msichana mmoja mrembo aitwaye Mwanaidi. Polisi wanawakamata watu wote waliokutwa humo, pamoja na wafanyakazi wa gesti hiyo kwa ajili ya mahojiano. Lakini inaonekana muda ambao walikuwapo wapenzi hao hakukuwa na mteja mwingine yeyote zaidi yao.

Baada ya mahojiano ya kina, inaonekana kabisa kuwa Mwanaidi ndiyo muuaji. Je, ni kweli? Kwa nini alimuua mpenzi wake wakiwa wamejifungia chumbani? Fuatilia hadithi hii kwa makini ambayo mbali na kukutia simanzi, furaha na kukuburudisha, pia itakufundisha, elimu na kufunulia mambo ambayo hukupata kuyafikiria kabla.

# Lazima apatikane-14

**Mtunzi anapatikana (0716 350534)**

**Na Adam Fungamwango**

Nilijitambulisha kwao kama mimi ni askari ili wasiwe na wasiwasi na maagizo yangu. Niliwapa kifuko cha plastiki ambacho vidonge vyake si sumu kama ulivyopewa wewe. Ndiyo maana mlipokwenda kaunta mlikaguliwa kwa namna isivyo kawaida. Pale walichokuwa wakitafuta ni hicho kifuko ambacho mimi niliwaambia kimo kwenye mkoba wako na wakabadilisha. Kile cha sumu wakakiondoa na kuweka nilichowapa mimi ambacho vidonge vyake vilikuwa vya kawaida, wakakurudishia mkoba bila wewe kujua na ndiyo maana hata ulipoviweka kwenye pombe ya Tika, alichofanya ni kulala fofofo tu, lakini hakufa."

"Samahani kwa sasa tumeambiwa ni lazima tusachi kwanza pochi, mikoba na vitu wanavyobeba wanaingia kwenye vyumba kwa sababu wengine wanakuwa na silaha, au vitu vya kuhatarisha wenzao, si mnakumbuka lile sakata la mtu kuuawa na mpenzi wake gesti lilivyotikisa?" Mwanaidi alikumbuka maneno ya mtu yule wa kaunta kabla ya kuingia na Tika.

"Yuko wapi sasa?"

"Wakati ule tayari nilikuwa nimeshaita askari wangu ambao niliwahadithia, nikawaambia akuache na wamchukue Tika kwa ajili ya mahojiano Makao Makuu ya Polisi, kwani ile dawa baada ya saa moja, usingizi unaondoka. Nadhani yeye ndiye atakuwa shahidi mzuri sana."

"Kumbe pale mimi niliona natoroka, mlikuwa mnaniona?"

Jan alitabasamu. "Ndiyo. Na niliwaambia wakuache makusudi kwa sababu nilijua ule mpango wa kutaka kujua muuaji wa Burhan sasa utakamilika muda si mrefu kwa sababu ndiyo ulikuwa mpango mama. Nilijua aliyekutuma kumuua Tika ni lazima akufuate, nikakufuata nyuma ili kuhakikisha usalama wako, lakini niliwahi kuingia humu kabla yako pia, ndipo Martin alipofuata."

"Sijui niseme nini Jan, wewe ni binadamu au malaika?"

"Mimi ni binadamu tu Mwanaidi."

"Sasa unaondoka saa hizi?"

"Ndiyo." Alijibu Jan na kutazama saa yake. Ilitimu saa nane usiku. "Usiondoke saa hizi, lala hapa hapa bwana." Mwanaidi alisema huku akimshika mikono yole miwili Jan kumzuia asiondoke.




"Unamuogopa mkeo atakuuliza?"

"Bado sijaoa."

"Basi lala usiku wa manane huu, mi naogopa kulala peke yangu bwana."

"Alfariji natakiwa niwe kazini." Jan aliongea kama mtu ambaye alitaka kusamu amri.

"Na mimi kesho ni siku yangu ya kuripoti huko huko kazini kwenu Makao Makuu kwa kesi yangu ya mauaji."

Jan alinyamaza. Akamtazama kwa Mwanaidi na makini. Mwanaidi alimtazama Jan akiwa anahema.

"Kesho tutaenda wote. Hebu njoo huku bwana." Mwanaidi alimvuta.

**********************************

Kilikuwa ni kikao. Si kizito sana. Lakini ni muhimu sana. Tayari Inspekta Msiya alikuwa amesharejea kutoka kwenye majukumu yake mkoani Kigoma. Ndiye awali aliyekuwa na faili la Mwanaidi.

Alipoondoka alimuachia afande kijana kabisa, Jan John faili la mwanamke huyo anayetuhumiwa kumuua mpenzi wake Burhan.

Wakati anaondoka aliona kila ushahidi unaonyesha kuwa Mwanaidi ni kweli alimuua Burhan. Alishangaa aliporudi kukuta haikuwa kweli.

Ni ukweli usiopingika kuwa hata ingekuwaje, asingeweza kumuondoa Mwanaidi kwenye mauaji hayo.

Kila mmoja alishangaa. Kila askari alishangaa kuona kibao kimegeuka. Msichana waliyedhani kuwa ni muuaji kumbe siyo.

Kumbe Burhan aliuawa na rafiki yake Martin baada ya kudhulumiana pesa. Mwanaidi aliingia kwenye dhahama hiyo kwa sababu tu ya kuwa ndani ya gesti na mpenzi wake. Martin aliingia kwa ujajusi wa hali ya juu bila mtu yoyote kuona, akamuua Burhan, akaondoka. Mwanaidi aliporejea kununua soda na kumkuta mpenzi wake ameuawa akazirai na kwenda kuzindukia hospitalini.

Kilichowashangaza askari wengi na hata Inspekta Msiya ni jinsi kitendawili kizito kilichojificha kuteguliwa na afande Jan.

Staili aliyotumia haikudhaniwa na wengi kuwa ingeweza kugeuza kutokana Mwanaidi kuwa muuaji, hadi kupatikana mtu mwingine kabisa ambaye hata hakuna ushahidi wowote ambao ungeweza kumnasa.

Maofisa kadhaa wa polisi walikuwa hapo wakitaka kujua ni kwa mbinu gani aliyotumia kumpata muuaji halisi wa Burhan ambaye baadaye ilikuja kujulikana kuwa ni jambazi.

Kwanza kabisa wanakumbuka alichoanza nacho ni kutaka msichana huyo apewe dhamana.

Ingewa ilikuwa ngumu sana kwa mtuhumiwa wa mauaji kupewa dhamana, lakini yeye aliwaambia yote hayo atayabeba yeye na hata kama ikiwa ni kupoteza kazi au kufungwa jela yupo tayari.

Leo hii Jan amegeuka kuwa shujaa, baada ya Jeshi la Polisi kumpata muuaji halisi wa Burhan, wakati dunia yote ikidhani ameuawa na mpenzi wake.

**Kilikuwa ni kikao. Si kizito sana. Lakini ni muhimu sana. Tayari Inspekta Msiya alikuwa amesharejea kutoka kwenye majukumu yake mkoani Kigoma. Ndiye awali aliyekuwa na faili la Mwanaidi.**

"Afande Msiya na maafande wenzangu wote, kitu cha kwanza baada ya kupokea faili hili na kumhoji mtuhumiwa mwenyewe wa kirefu, lakini pamoja na mazingira yenyewe, nilihisi kuna kitu ambacho kimejificha. Na kuomba kuachiwa kwenda nyumbani, nilitaka kutafuta kitu ambacho nilidhani kimejificha." Afande Jan aliwaambia wakubwa wake na maafande wengine.

"Kwanza kabisa nilianza kuwa na wasiwasi juu wa msichana kama Mwanaidi, ambaye ana miaka 25 tu nadhani kuwa na uwezo wa kushika kisu na kumuua mtu kama Burhan kwa kumchoma mara nne kifuani kwa uzito ule ule, kwani niligundua kuwa muuaji alitumia nguvu kubwa kudidimiza kisu mwilini. Kwa mwanamke wa kawaida, ambaye hana historia ya ujambazi au kuua, inakuwa si rahisi." Akasema na kuwafanya wenzake kuanza kupata somo ambalo hawakulijua kabla.

"Eti amemuua kisa tu ni milioni 100 zilizokuwa kwenye kifuko, lakini tukumbuke kuwa Burhan ni jambazi katili na mzoefu, isingewezekana mtu kama huyo kufanya kazi kubwa ya kupora, kuua wenzake watatu, halafu akaenda na mwanamke gesti, akakaa kizembezembe au kupitiwa na usingizi hadi kuchomwa kisu mara nne kirahisi vile. Nilianza kuhusi kuwa aliyemchoma kisu Burhan huenda naye alikuwa na uwezo na akili kama yeye. Hilo lilinifanya nianze kufikiri namna ya kutafuta namna nyingine ya kumtafuta mtu mwingine ambaye anaweza kuwa muuaji. Msichana kama Mwanaidi hata kama Burhan angelala usingizi, sidhani kama angemchoma kisu mara nne kwa nguvu ile ile bila woga wowote."

Koplo Hamisi na Inspekta Msiya walitazamana na kutikisa kichwa. Waliona kuwa kulikuwa na vitu fulani vya ndani ambavyo wao hawakuvitambua kabla.

"Ndiyo maana niliomba msichana huyu apewe dhamana. Nilijua yeyote ambaye yupo nyuma ya mpango huu atakuwa anamfuatilia. Na lengo lake ni kwamba Mwanaidi anyongwe au afungwe maisha ili yeye awe salama. Na kama ataachiwa, basi mtu huyo atamtafuta ili ammalize kwa ajili ya kupoteza ushahidi." Alinyanyua kikombe cha kahawa, akapiga mafunda kadhaa na kuweka mezani.

**ITAENDELEA JUMAMOSI**



# LINGARD AMSHUKURU SOUTHGATE

**LONDON, England**

NYOTA wa Manchester United, Jesse Lingard, amesema ushauri wa kocha wa Timu ya Taifa ya England, Gareth Southgate umemsaidia kumrudisha kwenye makali yake.

Lingard amesema kuwa kocha huyo amemwonesha msaada mkubwa na imani kubwa kwake na hasa kwa kumjumuisha kwenye kikosi cha England.


"Imani yake kwangu ni kubwa, alinipa nafasi kwa mara ya kwanza kwenye kikosi cha England, kitu ambacho najivunia," amesema akinukuliwa na talkSPORT.

"Ushauri wa Southgate ulihusika kwa kiasi kikubwa kwenye uamuzi yangu ya kujiunga na West Ham.

"Bado niliendelea kuwasiliana naye hata ingawa sikuwa nikicheza, ili tu kupata ushauri wake juu ya nini nifanye. Ilikuwa tu juu ya hoja sahihi, iwe ni kwenda timu nyingine za Ulaya au kubakia kwenye Ligi Kuu England.

"Aliniambia, 'Kama ningekuwa wewe, ningebaki kwenye Ligi Kuu'. Baada ya hapo, ilikuwa juu ya kutafuta timu ya Ligi Kuu England na West Ham ilionyesha nia." aliongeza.

# GRIEZMANN AMKOSOA KOCHA UFARANSA



**PARIS, Ufaransa**

ANTOINE Griezmann amehoji kuhusu mbinu za Ufaransa baada ya kulazimishwa sare ya 1-1 na Ukraine kwenye mchezo wa kwanza wa kufuzu Kombe la Dunia mwaka 2022.

Kocha mkuu wa Ufaransa, Didier Deschamps, alitumia mfumo wa 4-4-2 tofauti na ule ulizoeleka wa 4-2-3-1, mbinu ambayo haikuzaa matunda na kuleta hali ya maswali.

Griezmann alifunga bao la ufunguzi dakika ya 19 ya mchezo, lakini Ufaransa ilishindwa kuondoka na pointi zote tatu baada ya kusawazishwa kwa bao hilo.

Akizungumza na TF1, Griezmann alisema: "Labda tulihitaji wachezaji wasumbufu ambao wanauwezo wa kucheza mtu na mtu, tutajifunza kucheza kwa mfumo kama ambao unaleta matokeo.

"Tulihitaji kushinda lakini hatukucheza vizuri, tutaangalia na kujaribu kuboresha kwenye mchezo unaofuata.

"Tulipaswa kulinda ushindi wa kipindi cha kwanza, tulikuwa na nafasi na ilikuwa ngumu kwetu kipindi cha pili."

Baada ya mchezo wa Jumatano, Ufaransa watawakabili Kazakhstan hapo kesho Jumapili halafu watakutana na Bosnia na Herzegovina siku ya Jumatano ijayo.



# BARCELONA KUUZA NYOTA WANNE

**BARCELONA, Hispania**

KLABU ya Barcelona ina mpango wa kuwauza wachezaji wake wanne ili waweze kupata fedha kwa ajili ya kulipa madeni ambayo wanadaiwa, kwa mujibu wa El Confidencial.

Timu hiyo inadaiwa fedha nyingi kutokana na janga la virusi vya corona ambalo limefanya mapato wa timu nyingi duniani kushuka kwa sababu hakukuwa na mashabiki ambao wanaruhusiwa kuingia uwanjani, pamoja na shughuli za kiuchumi nyingi kusimama.

Majina ya wachezaji hao wanne ambao wamewekwa sokoni ni pamoja na Antoine Griezmann, Phillipe Coutinho, Samuel Umtiti na Francisco Trincao.

Coutinho ambaye alijiunga na Barca akitokea Liverpool mwaka 2018 kwa dau la pauni milioni 142, amecheza jumla ya mechi 90 na ametupia mabao 24, huku Griezmann bado hajawa kwenye ubora baada ya kuibuka ndani ya Camp Nou akitokea Atletico Madrid. Janga la corona limetibua mipango mingi ya timu mbalimbali duniani hasa kwenye uchumi na ilipeleka kupunguza mishahara ya wachezaji ndani ya Barcelona ili kuweza kupata nguvu ya kumudu gharama.

## HABARI MICHEZO



# MADRID
## YAKATAA KUMUUZA ODEGAARD

**LONDON, ENGLAND**

BAADA ya Arsenal kujiaminisha inaweza kuipata saini ya kiungo wa Real Madrid, Martin Odegaard, anayechezea kwa mkopo kwenye kikosi chao, Real Madrid wamesema kuwa hawafikirii kumuuza.

Arsenal ilimsajili Odegaard katika dirisha lililopita la majira ya baridi kwa usajili wa mkopo wenye thamani ya pauni milioni 1.8.

Mabao aliyofunga kwenye mechi dhidi ya Tottenham na Olympiacos, vilevile mchango wake katika kurudisha mabao kwenye mechi ya West Ham, imesababisha Kocha, Mikel Arteta kutamani zaidi kuipata saini yake ya kudumu.

Inaaminika Kocha wa Real Madrid, Zinedine Zidane anaamini zaidi kwenye uwezo wa fundi huyo na ndio maana alimpa nafasi ya kucheza kwenye kikosi chake cha kwanza lakini majeraha ya mara kwa mara ndio yalisababisha awe kwenye kiwango kibovu.

Taarifa kutoka tovuti ya Marca zinaeleza, Madrid ilikubali kumtoa kwa mkopo ili akaendelee kukomaa zaidi na baadaye ndio arudi kwenye kikosi, lakini sio kweli kwamba wanafikiria kumuuza.

Msimu uliopita fundi huyu alikuwa akiitumikia Real Sociedad kwa mkopo wa msimu mmoja ambapo alionyesha kiwango kikubwa kilichosababisha Madrid ikatae ofa ya Sociedad ya kumnunua mazima.

Akiwa na Arsenal msimu huu amecheza mechi 12 za michuano yote na kufunga mabao mawili.

# BLATTER AFUNGIWA TENA NA FIFA

**NYON, Uswisi**

AKIWA bado hajamaliza adhabu ya kifungo cha kutojihusisha na soka kwa muda wa miaka nane, Rais wa zamani wa Shirikisho la Soka la Kimataifa (FIFA), Sepp Blatter, amepewa adhabu mpya ya kifungo cha miaka sita itakayoanza mara baada ya adhabu ya sasa itakapomalizika.

Taarifa iliyotolewa na FIFA, imeeleza Blatter amekumbana na adhabu hiyo mpya baada ya kamati ya maadili kumkuta na hatia ya kuvunja kanuni za maadili za shirikisho hilo.

Blatter na aliyekuwa Katibu Mkuu wa FIFA, Jerome Valcke wanatuhumiwa kupokea zawadi ambazo zimetafsiriwa kama rushwa lakini pia matumizi mabaya ya ofisi pindi alipokuwa Rais.


"Uchunguzi dhidi ya Blatter na Valcke uligusa maeneo mengi yakiwamo malipo ya bonasi yanayohusiana na mashindano ya FIFA ambayo yalifanyika kwa viongozi wa juu wa FIFA," ilifafanua sehemu ya taarifa hiyo.

Lakini pia Blatter anatuhumiwa kutumia vibaya madaraka yake kwa kuidhinisha kiasi cha dola milioni 140 kwa ajili ya kurekebisha Makumbusho ya FIFA, kiasi ambacho ni zaidi ya gharama halisi za ukarabati huo.

Blatter amekuwa akikumbana na tuhuma mbalimbali ambazo zimepelekea afikishwe katika kamati ya maadili ya FIFA lakini hata mahakama za kawaida nchini Uswizi ambazo anadaiwa kujihusisha nazo pindi alipokuwa madarakani.

Novemba, mwaka 2017, kipa wa Timu ya Taifa ya Soka ya wanawake ya Marekani, Hope Solo alimtuhumu Blatter kuwa alimfanyia udhalilishaji wa kingono katika hafla ya tuzo za FIFA Ballon d'Or mwaka 2013.

# COSTA ATUA RASMI BENFICA



**LISBON, URENO**

DIEGO Costa amefikia makubaliano na Benfica kwa ajili ya kujiunga na miamba hiyo ya soka Ureno, huku ikitajwa kuwa mshambuliaji huyo wa zamani wa Chelsea anaweza kusaini mkataba wa miaka miwili wenye thamani ya pauni milioni tano.

Desemba mwaka jana, mshambuliaji huyo mwenye asili ya Brazil, aliachana na Atletico Madrid baada ya kufanyika makubaliano ya pande zote mbili.

Gazeti kubwa na maarufu huko Hispania, Mundo Deportivo limeripoti kwamba Costa alikuwa na mpango wa kurudi Brazil lakini amebadili uamuzi na kuamua kubaki Ulaya baada ya kufikia makubaliano na Benfica.

Costa mwenye umri wa miaka 32 sio kwamba hakuwa na ofa ya kucheza miongoni mwa zile Ligi kubwa zaidi Ulaya, inaelezwa kwamba aliigomea Marseille ya Ligi Kuu Ufaransa.

Mtukutu huyo ambaye alitupilia mbali nafasi ya kuichezea timu ya taifa la Brazil na kuchagua Hispania, ameamua kurejea zake, Ureno ambako miaka ya nyuma alikuwa akiichezea Braga kabla ya kutua Atletico Madrid, 2007.

Inasemekana kuwa Benfica imempa ofa ya Pauni milioni 2.6 kwa msimu ili aichezee timu hiyo, licha ya kiwango kidogo cha fedha, alikubaliana nao.

Jambo lingine ambalo limetajwa kuchangia kufikia pazuri kwa uhamisho huo ni kutokana na ukaribu uliopo baina ya wakala wake, Jorge Mendes na klabu kutoka Ureno.

HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# BARCELONA YAJITOSA KUMWANIA HAALAND

Ni baada ya kocha wake Koeman kumtaja ni mchezaji ambaye ni kipaumbele katika usajili...

**BAECELONA, Hispania**

KOCHA wa Barcelona, Ronald Koeman, amemtaja nyota wa Borussia Dortmund, Erling Haaland kama mchezaji ambaye ni kipaumbele chake kikubwa kwenye usajili wa kipindi cha majira ya joto, kwa mujibu wa Diario AS.

Kwa maana hiyo, Barcelona imejiunga kwenye mbio na klabu nyingi za kuwania saini ya nyota huyo, ambaye anaonekana kuwa lulu barani Ulaya kwa sasa.

Haaland amekuwa akitwaja na klabu nyingi barani Ulaya kumwania kutoka kwa miamba hao wa Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga na sasa Barca wameamua kujitosa rasmi.

Kwa mujibu wa ripoti Koeman anaona Halaand anafiti zaidi kwenye kikosi hicho ambacho kwa sasa kinapambana kuhakikisha kinasajili nyota wengi wakati wa dirisha la kipindi cha majira ya joto kinachokuja.

Koeman anataka kuimarisha kikosi chake hicho kwenye safu ya ushambuliaji, baada ya kuwa na msimu mbaya wa kutolewa mapema kwenye mashindano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu huu.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Norway amekuwa na wakati mzuri zaidi kule Bundesliga na sasa Barca wanafanya kila liwezekanalo kuhakikisha wanamtwaa nyota huyo.

Haaland amekuwa akihusishwa na klabu kadhaa zikiwamo, Real Madrid, Manchester City, Chelsea, Paris Saint-Germain, Juventus na Liverpool.

Koeman pia ameripotiwa anamtaka mlinzi wa City, Eric Garcia, nahodha wa Lyon, Memphis Depay na kiungo wa Liverpool, Georginio Wijnaldum.

## KWA UFUPI

**MESSI KUBAKI BARCA**

NYOTA wa Argentina, Lionel Messi mwenye umri wa miaka 33, yuko tayari kusaini mkataba mpya na Barcelona kufuatia uchaguzi wa rais mpya Joan Laporta, kwa mujibu wa gwiji straika wa zamani wa Barcelona, Rivaldo. ***(The Sun)***

**ODEGAARD AOTA MBAWA**

ARSENAL hawana fursa ya kumsajili kwa mkataba wa kudumu nyota wa Real Madrid anayecheza hapo kwa Martin Odegaard mwenye umri wa miaka 22.

**WIJNALDUM KUSUBIRI**

KIUNGO wa kati wa Liverpool, Georginio Wijnaldum mwenye umri wa miaka 30, atahitaji kusubiri hadi Barcelona watakapomwachia, Miralem Pjanic mwenye miaka 30, kabla hajakamilisha mkataba wake wa kuhamia pale Nou Camp. ***(Sport via Mirror)***

**LUKAKU ANUKIA BARCA**

MSHAMBULIAJI wa Inter Milan na Ubelgiji, Romelu Lukaku mwenye umri wa miaka 27, analengwa na kocha wa klabu ya Barcelona, Ronald Koeman. ***(Calcio Mercato)***

**LIVERPOOL YAMTAKA MALEN**

LIVERPOOL wanaangalia uwezekano wa kumsajili mchezaji wa PSV Eindhoven, Donyell Malen, licha ya kinda huyo mwenye umri wa miaka 22 raia wa Uholanzi kusakwa na timu kubwa za Italia, Juventus na AC Milan. ***(Gazzetta Dello Sport via Goal)***

**SOLSKJAER KUULA ZAIDI**

KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer mwenye umri wa miaka 48, anatarajiwa kusaini mkataba mpya hata kama timu hiyo itamaliza bila taji msimu huu. ***(Telegraph - subscription only)***

**WILDER HAKUFUKUZWA**

MMILIKI wa klabu ya Sheffield United, Prince Abdullah amesema hakutaka kumfukuza kocha, Chris Wilder. ***(Sky Sports)***

**IHEANACHO MAMBO SAFI**

MSHAMBULIAJI wa Timu ya Taifa ya Nigeria, Kelechi Iheanacho mwenye umri wa miaka 24, yuko tayari kusaini mkataba mpya na Leicester City msimu huu. ***(The Sun)***

**TOTTI AGEUKIA UWAKALA**

MKONGWE wa AS Roma, Francesco Totti mwenye umri wa miaka 44, anaweza sasa kufanya kazi kama wakala wa michezo baada ya kukamilisha taratibu za kujiuzulu kwake nchini Italia. ***(Gazzetta dello Sport - in Italian)***

**SILVA ATAKIWA BARCA**

BARCELONA wanamtaka mchezaji wa Eintracht Frankfurt, Andre Silva, raia wa Ureno mwenye umri wa miaka 24. ***(Marca)***

**RODRIGUEZ SOKONI**

KIUNGO wa kati wa Real Betis na Argentina, Guido Rodriguez mwenye umri wa miaka 26, amesema anatambua kuhusu taarifa zilizoripotiwa kuwa Arsenal wanawania saini yake. ***(Evening Standard)***

HABARI MICHEZO

# MWAMBUSI ALILIA MECHI ZA KIRAFIKI

**Na Saada Akida**

ILI kuimarisha kikosi chake, Kaimu Kocha Mkuu wa Yanga, Juma Mwambusi, ameweka wazi anahitaji mechi za kirafiki mbalimbali ili kukiweka tayari kikosi chake kabla ya kurejea kwa Ligi Kuu Tanzania Bara na mashindano ya Kombe la FA.

Kwa sasa Yanga inaendelea na mazoezi katika kambi yao iliyopo Kigamboni kwenye viwanja vya Avic kujiandaa na mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Biashara United unaotarajiwa kuchezwa Aprili 11, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, jijini Dar es Salaam. Lakini pia inajiandaa na mchezo wa raundi ya tano wa Kombe la FA dhidi ya Tanzania Prisons utakaochezwa kwenye Uwanja wa Nelson Mandela ulioko Sumbawanga baadaye mwezi ujao.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Mwambusi alisema anaamini michezo ya kirafiki atakayopata itamsaidia kukipima kikosi chake na kufikia malengo yake ya kufanya vyema msimu huu.

Mwambusi alisema mechi hizo zitasaidia kuwajenga imara wachezaji wake kwa sababu amesharidhishwa na stamina waliyonayo tangu aliporejea kwenye kikosi hicho akichukua mikoba ya Mrundi Cedric Kaze.

"Kufanya mazoezi ni tofauti na kupata mchezo wa kirafiki, nina imani ningepata hata mechi moja ingenisaidia, kutokana na msiba mzito wa Taifa, nina asilimia ndogo ya kupata, kutokana na ratiba kubana."

"Kwa sasa tuko katika maombolezo na michezo yote ya ndani imesimama kwa ajili ya kupisha maombolezo hata baada ya kumalizika kwa maombolezo hayo, hatutapata muda mwingine wa kucheza mchezo wowote wa kirafiki kwa sababu tunahitaji kuendelea na Ligi Kuu pamoja na Kombe la FA," alisema Mwambusi.

Alisema bado wanasubiri kufahamu siku watakayocheza dhidi ya KMC FC ambayo kwa ratiba ya awali ulipangwa kuchezwa Aprili 7, mwaka huu siku ambayo itakuwa ndio mwisho wa maombolezo ya msiba wa Rais. Dk. John Pombe Magufuli.

"Nitaendelea kutumia mazoezi ya wenyewe kwa wenyewe kuangalia utimamu wa wachezaji wangu, huku nikiwa na matumaini ya nyota waliokuwa majeruhi wanarejea vizuri ikiwamo Fiston Abdulrazack ambaye ameanza mazoezi mepesi," alisema Mwambusi.

Aliongeza wamejiandaa kukabiliana na ushindani kwa sababu katika hatua iliyofikia kila timu inahitaji kukamilisha malengo yake.

Yanga itarejea katika Ligi Kuu Tanzania Bara ikiwa na kumbukumbu ya kutoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Polisi Tanzania, katika mchezo huo ulioisha sare ya bao 1-1, bao la Yanga likifungwa na Fiston na Pius Buswita aliisawazisha timu yake hiyo inayotumia Uwanja wa Ushirika ulioko mkoani Kilimanjaro.



Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Klabu ya Simba, Haji Manara (mwenye kofia), akiwa na baadhi ya wasanii wa filamu nchini katika mazishi ya aliyekuwa Rais wa Tanzania, Dk. John Pombe Magufuli ambaye alizikwa nyumbani kwao Chato mkoani Geita jana. **PICHA: MTANDAO**

# Gaucho rasmi asajiliwa Morocco

**Na Saada Akida**

ALIYEKUWA mshambuliaji wa Simba Queens, Mwanahamisi Omari, `Gaucho` sasa rasmi ni mali ya klabu ya Chabab Atlas Khenifra Femine, (CAK SC) inayoshiriki Ligi Kuu ya Wanawake nchini Morocco, baada ya kusaini mkataba wa miaka miwili na nusu, imefahamika.

Akizungumza na gazeti hili jana, Ofisa Uendeshaji wa Simba, Anold Kashembe, alisema tayari mazungumzo ya kukamilisha uhamisho wa Gaucho yamekamilika na wameshawatumia CAK SC kibali (ITC) ya mshambuliaji huyo.

Kashembe alisema uongozi wa Simba umempa baraka zote nyota huyo wa Timu ya Taifa ya Wanawake (Twiga Stars) na wanamtakia mafanikio kwenye klabu yake hiyo mpya. "Tumeshamalizana na uongozi wa CAK SC, sasa Mwanahamisi ni mchezaji halali wa klabu hiyo ya nchini Morocco, baada ya pande zote tatu kufikia mwafaka na nyota huyo kusaini mkataba wa miaka miwili na nusu," alisema Kashembe.

Aliongeza kuondoka kwa mshambuliaji huyo kutatoa fursa kwa wachezaji wengine kupata nafasi ya kutoka kwenda kucheza soka la kulipwa nje ya Tanzania.

"Tunaimani Mwanahamisi atakuwa amefungua milango ya wachezaji wengine wa kike kucheza soka la kulipwa, hivyo endapo itatokea nafasi ya mchezaji mwingine na maslahi kwa pande zote, tutamruhusu kwenda kujaribu bahati yake kama ilivyo kwa nahodha wetu huyo," alisema Kashembe.

## Chikwende aipeleka Zimbabwe AFCON

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI Tanzania ikiugulia maumivu ya kushindwa kufuzu Fainali za Mataifa ya Afrika (AFCON) kwa kuchapwa bao 1-0 dhidi ya Equetorial Guinea, straika wa Simba, Perfect Chikwende, alifunga bao pekee lililoipeleka Zimbabwe kwenye fainali hizo zitakazofanyika mwakani nchini Cameroon.

Chikwende aliyesajiliwa na Simba kipindi cha dirisha dogo akitokea FC Platinum ya nchini humo, alifunga bao dakika ya 15 ya mchezo na kuifanya Zimbabwe iliyokuwa ugenini Botswana kufuzu AFCON.

Straika huyo alifunga bao hilo kwa kichwa, baada ya faulo iliyopigwa na Knowledge Musona na kuifanya Zimbabwe kufikisha pointi nane kwenye Kundi H ambazo hazitoweza kufikiwa na timu za Botswana na Zambia ambazo zote zina pointi nne.

Zimbabwe imefanikiwa kutinga AFCON ikiwa kwenye nafasi ya pili ya kundi hilo linaloongozwa na Algeria ambayo nayo imeshafuzu, ikitoka sare ya mabao 3-3 dhidi ya Zambia juzi kwenye mechi iliyochezwa mjini Lusaka.

Kiungo wa Simba, Clatous Chama ni mmoja kati ya wafungaji wa Zambia, mawili yakifungwa kwa mkwaju wa penalti na Patson Daka, mabao ya Algeria yakifungwa na Islam Slimani aliyefunga mabao mawili na Rachid Ghezzal.

## Polisi Tanzania yaiwaza Azam

**Na Shufaa Lyimo**

KOCHA Mkuu wa Polisi Tanzania, Malale Hamsini, amesema 'akili na mawazo' yote ameyaelekeza katika mchezo wao wa Kombe la FA dhidi ya Azam FC utakaochezwa kwenye Uwanja wa Azam Complex jijini Dar es Salaam.

Malale aliliambia gazeti hili licha ya sasa kuwa kwenye maombolezo ya msiba wa aliyekuwa Rais, Dk. John Pombe Magufuli, kikosi chake kimeanza mazoezi kwa ajili ya kutafuta 'dawa' ya ushindi dhidi ya wenyeji hao wa Chamazi.

Kocha huyo alisema amejipanga kuwapa mbinu mpya wachezaji wake kwa kutambua watakutana na timu ngumu na yenye wachezaji wazuri na wazoefu.

"Tunaitafutia dawa Azam mapema kwa sababu tunafahamu ni moja kati ya timu ambayo ina wachezaji wazuri hivyo tutakapokutana nayo tunatakiwa tuingie kwa tahadhari kubwa ili wasipate nafasi ya kutufunga kiurahisi,"alisema Malale.

Aliongeza wanatumia vyema siku za mapumziko kujiimarisha kwa sababu msimu huu wanahitaji kumaliza katika nafasi nne za juu kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Michezo
Jumamosi Machi 27, 2021
Nipashe



BARCELONA YAJITOSA KUMWANIA HAALAND

HABARI UK 22

# STARS YAJIPANGA KULINDA HESHIMA

●●●Ni baada ya kushindwa kumuenzi vyema Magufuli kwa kuondolewa katika…

**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), kushindwa kumuenzi vyema aliyekuwa Rais wa Tanzania Dk. John Pombe Magufuli, kwa kukosa tiketi ya kushiriki Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON), kikosi hicho kimejipanga kulinda heshima kwenye ardhi ya nyumbani.

Juzi usiku Stars ilikubali kichapo cha bao 1-0 kutoka kwa Equatorial Guinea na kupoteza nafasi ya kufuzu AFCON baada ya kubakia na pointi nne ikishuka dimbani katika michezo mitano wakati kinara wa Kundi J akiwa ni Tunisia yenye pointi 13.

Equatorial Guinea iliyofikisha pointi tisa iko katika nafasi ya pili, Taifa Stars ni ya tatu na Libya yenye pointi tatu ikiburuza mkia kwenye kundi hilo.

Bao pekee la Equatorial Guinea katika mechi hiyo iliyochezwa kwenye Uwanja wa Nuevo do Malabo lilifungwa na nahodha wake, Emilio Nsue Lopez dakika ya 90.

Hata hivyo ikumbukwe mwaka juzi Rais Magufuli akiwa kiongozi wa nchi, Taifa Stars iliyokuwa chini ya Kocha Mkuu Mnigeria Emmanuel Amunike ilikata tiketi ya kushiriki fainali hizo kwa mara ya pili, baada ya kukosa nafasi hiyo kwa miaka 39.

Stars iliyoko chini ya Kocha Mkuu, Kim Poulsen inatarajia kukamilisha ratiba kwa kuwakaribisha Libya hapo kesho kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Clifford Ndimbo aliliambia gazeti hili jijini jana kuwa kikosi kimerejea salama nchini na kitaendelea na mazoezi kwa ajili ya mchezo wao wa mwisho wa Kundi J dhidi ya Libya.



Mshambuliaji wa Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), Iddi Selemani 'Nado' (kulia), akijiandaa kumtoka mchezaji wa Equatorial Guinea, katika mechi ya Kundi J ya kusaka tiketi ya kushiriki Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON), iliyochezwa juzi usiku. Stars ililala bao 1-0. **PICHA: TFF**

Ndimbo alisema hali ya wachezaji wa timu hiyo ni nzuri na watauchukulia 'uzito mkubwa' mchezo huo licha ya tayari wamepoteza nafasi ya kushiriki fainali zijazo za AFCON.

"Tunawatarajia kuwasili nchini saa 12:00 jioni ya leo (jana)," alisema kwa kifupi Ndimbo.

Mechi kati ya Stars dhidi ya Libya itachezwa kuanzia saa 10:00 jioni na kwa mujibu wa maelekezo kutoka katika Shirikisho la Soka Afrika, mchezo huo utafanyika bila ya mashabiki.

Mechi hiyo itakuwa ni ya kwanza kuchezwa nyumbani huku nchi ikiwa kwenye kipindi cha siku 21 za maombolezo kufuatia msiba wa aliyekuwa Rais, Dk. Magufuli ambaye alizikwa nyumbani kwao Chato mkoani Geita jana.

Baada ya mchezo huo, wachezaji watarejea katika klabu zao kwa ajili ya kuendelea na maandalizi ya mechi za mashindano ya Kombe la FA na michezo ya Ligi Kuu Bara msimu wa 2020/21 iliyosalia.

## SERIKALI YAWASHUKURU WASANII, WADAU WOTE

**Na Maulid Mmbaga**

WAKATI Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, akiwashukuru wasanii wote wa hapa nchini kwa kuimba nyimbo mbalimbali za maombolezo kufuatia msiba wa aliyekuwa Rais, Dk. John Pombe Mafuguli, wanamichezo wameendelea kumlilia kiongozi huyo aliyezikwa nyumbani kwao Chato mkoani Geita jana.

Majaliwa alisema katika hotuba yake nyimbo zilizoimbwa na wasanii hao ziliongeza utulivu katika kipindi hichi cha msiba na aliwasifu kazi waliyoifanya ilikuwa ni nzuri.

Alisema nyimbo hizo zimewapa faraja Watanzania ambao wataendelea kumkumbuka Rais Magufuli kwa mambo mbalimbali aliyoyafanya ndani ya kipindi chake cha uongozi.

Mwenyekiti wa Chama cha Wachezaji wa Soka Tanzania (SPUTANZA), Mussa Kisoki alisema Rais Magufuli alifanya mambo mengi ya maendeleo lakini kwa upande wa wanamichezo waliamini alikuwa ni mtu aliyependa kuona maendeleo ya mpira wa miguu yanapatikana kwa haraka.

Kisoki alisema marehemu aliupa kipaumbele mchezo wa soka na anaimani Rais, Samia Suluhu Hassan pia ataendeleza pale ambapo hayati Magufuli alipaacha katika kulipeleka mbele taifa kimichezo.

"Ninaamini Rais Samia pamoja na wasaidizi wake akiwamo Waziri wa Michezo (Innocent Bashungwa), watakaa pamoja kuendeleza mazuri yaliyopo, lengo la kila Mtanzania ni kuona nchi inafika kule mbele kunakohitajika kwa ajili ya maendeleo ya soka," alisema Kisoki.

Kocha wa makipa wa Timu ya Taifa (Taifa Stars), Saleh Machupa alisema watamkumbuka Rais Magufuli kama mmoja wa watu waliokuwa wanapenda michezo na alitamani kuona inapiga hatua kimaendeleo.

"Hata Timu ya Taifa ilipokwenda AFCON mwaka juzi alitoa mchango mkubwa sambamba na kutoa 'bonasi' kwa kila mchezaji jambo ambalo hakuna mtu atakayeweza kumsahau kwa kitu alichokitoa," alisema Machupa. Naye meneja wa Stars, Nadir Haroub 'Cannavaro' alisema Rais Magufuli alijitolea kuinua michezo na sanaa huku pia alidhamiria kuwasaidia na kulifikisha taifa mbali kwenye sekta hiyo.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002